# Nipashe

Jumanne Desemba 26, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581536

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



Nipashe TESA

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Kutoka kuazima ardhi hadi kumiliki shamba la miti

Msongamano, foleni barabarani ulivyotesa 2023, kuendelea tena

NA SABATO KASIKA

Karibu mwaka 2024, wadau elimu wanatamani kufeli 'English' kukome

UKURASA 11

**DC**, AG waitwa mahakamani mgogoro wa jengo la kanisa

UKURASA 8

**Upinzani** waja juu zabuni za miradi Zanzibar kutotangazwa

UKURASA 17



**Papa** atoa ujumbe maalum yanayojiri Gaza, Ukraine, Russia

UKURASA 19

# Maaskofu wang'aka

• **WASEMA** heri kubariki jiwe kuliko ndoa ya jinsia moja. Shoo alia na afya ya akili, ripoti za CAG... *Endelea Ukurasa 2 & 3*



Dk. Flavian Kassala

"Ndoa ya jinsia moja ni kinyume cha agano la Mungu. Kwangu ni bora nikabariki jiwe likajenge na si uchafu huo."



Dk. Shoo

"Ubadhirifu na ukwapuaji fedha unaotokea, hasa katika halmashauri. Ripoti za CAG zinasikitisha. Sasa hivi kuna kilio cha afya ya akili. Shida ni...



Askofu Antony Lagwen

"Kanisa Katoliki halitabariki wale waliokengeuka katika suala la maadili.

# Wamiliki hospitali binafsi watishia kutopokea wenye bima za NHIF

UKURASA 8

RIPOTI YA UCHUNGUZI

## MJAMZITO ALIYEBAKWA...

# Polisi Mkuranga wazua jambo



• **PIKIPIKI** iliyonaswa eneo la tukio, yaachiliwa... *Uk. 4*

**MICHEZO** SIMBA SC, YANGA ZAANDAA 'SUPRISE' UK.24 **MAONI** UK.6

# Dk. Mpango Acheni kutupa vichanga na kutoa mimba

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na mkewe, Mbonimpaye Mpango jana waliungana na waumini wengine nchini katika ibada ya Sikukuu ya Krismasi, akikemea utupaji vichanga na utoaji mimba.

Alishiriki ibada hiyo katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mwenyeheri Maria Theresa Ledochowska Kiwanja cha Ndege, mkoani Dodoma, ikiongozwa na Paroko wa Parokia hiyo, Padre Emmanuel Mtambo.

Akitoa salamu za sikukuu ya Krismasi kupitia kwa waumini hao, Makamu wa Rais aliwasihi Watanzania kusherehekea sikukuu kwa amani na utulivu pamoja na kujitoa kusaidia wasio na uwezo wakiwamo yatima.

Makamu wa Rais pia alitoa wito kwa Watanzania kuwalea vyema watoto na kuwaongoza katika kumjua Mungu, kuwafundisha uzalendo na kufanya kazi kwa bidii, kuwaongoza katika kuipenda nchi na kuitumikia wakiwa raia na baadaye kuwa viongozi waadilifu.

Dk. Mpango pia aliwaasa Watanzania kuendelea kupinga aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Alisema ni vyema sikukuu ya Krismasi ikatumika kujitafakari na kuachana na tabia za kutupa watoto pamoja na utoaji mimba.

Vilevile, Makamu wa Rais aliwaomba waumini na viongozi wa dini kuendelea kuliombea taifa ili amani idumu na kuepushwa na mafarakano.

Pia aliwataka Watanzania kujiandaa ili kushiriki vyema katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwakani pamoja na kuliombea taifa kupata viongozi walio bora.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Johansen Kahatano (mbele), akizungumza na waandishi wa habari juzi, baada ya kufanya ukaguzi wa nauli katika mabasi stendi ya Arusha kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Askofu Shoo aanika kilichojificha wengi kukumbwa tatizo afya akili

**Na Waandishi Wetu**

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amesema hivi sasa kuna kilio kikubwa nchini kuhusu tatizo la wagonjwa wa afya ya akili.

Amesema tatizo hilo limesababishwa na watu wengi kukosa hekima ya kuwa na kiasi na kujua ni nini kilicho cha muhimu zaidi katika maisha.

Mifano halisi juu ya tatizo hilo, Dk. Shoo amesema inachagizwa na taarifa nyingi za ubadhirifu na ukwapuaji fedha unaotokea na hasa katika halmashauri, ambako serikali imetenga mabilioni ya shilingi kwa ajili ya kugharamia miradi ya elimu, maji, afya na barabara.

Aliyasema hayo jana wakati wa ibada ya Sikukuu ya Krismasi iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini.

Dk. Shoo alisema, "neema ya Mungu ituwezeshe kuishi kwa kuwa na kiasi. Watu wengi wamekuwa na mahangaiko makubwa kwa kukosa kuwa na kiasi katika maisha.

"Kuwa na kiasi na kujua ni nini kilicho cha muhimu zaidi katika maisha yetu, ni nini kinachonitosha katika maisha haya, ni ipi iwe mipaka yangu ya uwezo wangu ya kuishi kwangu, ni hekima kubwa na tukijaliwa hilo ni neema kubwa sana.

"Ninajua wako watu sasa hawana amani katika mioyo yao kwa sababu wamekosa tu ile hekima ya kuwa na kiasi katika maisha yao. Iwe ni mali, iwe ni madaraka na kitu chochote, kuwa na kiasi ni neema ya Mungu, ambayo kwa wale waliompokea kristo, huyu mwana wa Mungu wanapaswa kuwa nayo."

Dk. Shoo ambaye ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, alisema taarifa nyingi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zinasikitisha, hasa unaposikia juu ya ubadhirifu na anachokiita ukwapuaji unaotokea na hasa katika halmashauri.

Kutokana na kukithiri kwa tamaa, Askofu Dk. Shoo aliwaomba viongozi wa umma na watendaji kuwa na roho ya uzalendo na wawe watu wanaopenda kutenda haki.

Kuhusu tatizo la ongezeko la watu wenye ugonjwa wa afya ya akili, Mkuu wa KKKT alisema, "sasa hivi kuna kilio cha afya ya akili. Hii inatokana na nini? Kwa sehemu kubwa ni watu kutokujua ni nini cha muhimu katika maisha yao. Sababu yake kubwa ni kutokuwa na kiasi katika maisha.

"Kuna mahangaiko katika jamii, kuna mapigano katika jamii duniani, ni kwa sababu tumeacha kutendeana haki. Yesu Kristo atusaidie kutamani kutenda yaliyo ya haki, usimtendee mwanadamu mwenzako kile ambacho wewe mwenyewe hupendi kutendewa.

"Tutendee haki nafasi tunazozipata; iwe ni madaraka, iwe ni nafasi katika familia, tuwe watu wenye kutenda haki.

"Tunapokea taarifa nyingi za watu wanapewa dhamana, anapewa nafasi katika jamii kwa maana ya kutunza mali za umma, lakini utasikia habari nyingi tu za ubadhirifu, ambapo kwa wachache kutumia nafasi zao vibaya wanakwapua pesa (fedha) ambazo zimetolewa na serikali kwa ajili ya kuwaletea wananchi maendeleo."

### UTAJIRI VIJIWENI

Naye Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Arusha, Mhashamu Askofu Isaac Amani, amewaonya vijana wenye tabia ya kupenda mafanikio kwa njia ya miujiza na kukaa vijiweni, akiwataka waachane na ndoto hizo na badala yake wajikite katika kuchapa kazi kwa bidii ili kupata mafanikio wanayohitaji.

Akihubiri katika Kanisa la St. Theresia, Askofu Amani, alisema tabia ya vijana kukaa vijiweni, huku wakisubiri miujiza ya kupata utajiri ni mbaya na inapaswa kukemewa na kila mmoja.

Pia aliwataka wazazi kusimamia watoto wao ili wawe na afya njema ya akili na maadili mema kwa ajili ya kulipigania taifa lao.

"Siku hizi wazazi wanaachia watoto wao kulelewa na wafanyakazi na mitandao ya kijamii, ambayo huko hujifunza tabia zisizo njema na maadili mabovu, ambayo kimsingi si utamaduni wetu na matokeo yake tunaanza kulalamika siku hizi kuna mmomonyoko wa maadili," alisema.

### UZINZI, UASHERATI

Askofu Mkuu wa Kanisa la The Free Pentecostal Church of Tanzania (FPCT), Stevie Mulenga, amekemea vitendo vya uasherati, ulevi, wizi, akisema vinaweza kusababisha madhara makubwa kwa jamii, ikiwamo kupoteza maisha.

Askofu Mulenga alisema, "siku ya Sikukuu si lazima watu wavae nguo mpya, lakini nikemee pia vitendo vya uzinzi, ulevi, wizi na uasherati ambavyo vinaweza kusababishia madhara makubwa kwa jamii ikiwamo kupoteza maisha na kuwaacha wenza."

Alisema kuwa wakati Watanzania wakikaribia kuumaliza mwaka 2023, wanapaswa kuendelea kuitunza amani na kuendelea nayo kwa sababu ndio tunu kubwa ya taifa.

"Wakati tunakaribia kumaliza mwaka, kuna wenzetu wako hospitalini, wengine wapo kwenye vita lakini sisi Watanzania Mungu ametupa uzima na afya na kutuepusha na vita, hivyo ni vizuri tuendelee kuenzi amani yetu," alisisitiza.



IBADA YA KRISMASI

# Maaskofu: Ni heri kubariki jiwe kuliko ndoa jinsia moja

Na Waandishi Wetu

MAASKOFU na wachungaji wa madhehebu ya dini nchini wamesisitiza Watanzania kudumisha amani, utulivu na kukemea ndoa za jinsia moja.

Vilevile, wamewakumbusha wazazi kuwalea watoto katika maadili mema, kutokaribisha viashiria vya udini na ukabila.

Katika mahubiri ya sikukuu ya Krismasi jana, viongozi hao pia waliwakumbusha Watanzania kuwakumbuka kwa misaada na ushauri watu wenye matatizo na wenye uhitaji wa misaada.

Rais wa Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania (TEC), Gervas Nyaisonga, aliwataka Watanzania kuendelea kudumisha amani na utulivu uliopo ili kuendelea kuwa nchi ya mfano duniani.

Askofu Nyaisonga ambaye ni Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mbeya aliyasema hayo wakati akihubiri kwenye mkesha wa sikukuu ya Krismasi uliofanyika Kanisa Kuu Katoliki la Mtakatifu Anthony wa Padua jijini Mbeya.

Alisema kuwa katika kusherehekea sikukuu ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo, ni wakati wa kuhimizana kutenda mambo mema ambayo hayawezi kusababisha mifarakano kwenye jamii.

"Huu ni wakati wa kubadilika, tuhakikishe tunatenda mambo mema ya kumpendeza Mungu, lakini tuhakikishe tunaliombea taifa letu liendelee kuwa na amani, tuepuke mifarakano kwenye jamii zetu," alisema Askofu Nyaisonga.

Akihubiri katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Forest Jimbo la Mgharibi Dayosisi ya Konde, Askofu Mkuu wa Dayosisi hiyo, Geofrey Mwakihaba, mbali na kuhimiza amani na utulivu, pia aliwataka Watanzania kuendelea kukumbuka watu wenye uhitaji.

Askofu Mwakihaba aliwataka Watanzania kuendelea kuombea watu waliopata majanga, wakiwamo wakazi wa mji wa Katesh wilayani Hanang' mwanzoni mwa mwezi huu walikumbwa na janga la maporomoko ya tope, magogo na mawe yaliyosababisha vifo vya zaidi ya watu 80.

Alisema watu hao pamoja na wa maeneo mengine yaliyokumbwa na maafa, wanahitaji faraja hasa katika kipindi hiki ambacho ni cha kusherehekea sikukuu ya Krismasi.

Vilevile, askofu Mwakihaba aliwataka Watanzania kuwalea watoto wao katika maadili mema ikiwa ni pamoja na kuwafundisha kusali ili wakue wakimjua Mungu.

"Wakati huu wa sikukuu ni wakati wa kufurahi, lakini ninawaomba msiwaruhusu watoto kwenda kwenye nyumba za starehe, hakikisheni mnawafundisha kutenda mambo mema," alisema Mwakihaba.

NDOA JINSIA MOJA

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Mbulu, Antony Lagwen, katika mahubiri yake, alisema kanisa hilo linatambua ndoa za mume na mke mmoja na si vinginevyo kama ambavyo mitandao ya kijamii inasema.

"Tafsiri zinazotolewa kanisani, zinatolewa kwa wote, hivyo Kanisa Katoliki halitabariki wale waliokengeuka katika suala la maadili kama mitandao inavyoeleza," alisema Lagwen.

Alisema wananchi wanatakiwa kuwajibika vizuri kwa ngazi zote katika kupinga ukatili unaoendelea kwenye jamii kwa kuwalinda watoto.

Naye Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Geita, Dk. Flavian Kassala ambaye ni Makamu wa Rais wa TEC, alisema hayuko tayari kubariki ndoa ya jinsia moja, akisema ni kinyume na agano la Mungu.

Dk. Kassala alisema ni bora abariki jiwe ili likatumike kujenga nyumba na si kubariki watu wa jinsia moja wanaotaka kufunga ndoa katika kanisa hilo.

Askofu Kassala alisema kubariki ndoa ya jinsia moja ni kwenda kinyume cha maandiko ya Mungu.

"Binadamu amemwacha Mungu na kufanya mambo yake yanayokwenda kinyume cha kuendeleza uumbaji.

"Wanaharibu vizazi kwa kutoa mimba na sasa wanataka tubariki ndoa za jinsia moja.Kwangu ni bora ni kubariki jiwe na siyo uchafu huo," alisisitiza Askofu Dk. Kassala.

Pia alikemea na kuonya kuhusu kuendekeza udini na ukabila katika masuala mbalimbali ya kitaifa na kuwataka wanaoendekeza vitu hivyo kuacha ili kulinda tunu ya amani iliyopo nchini kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye.

Alisema baadhi ya mataifa yaliyochezea amani kwa kuendekeza masuala ya udini na ukabila, leo wanapiga vita kila kukicha.

Aliwataka Watanzania kutokubali kutenganishwa kwa udini, ukabila na itikadi za siasa. Baadhi ya nchi ziliingia kwenye machafuko kutokana na kuendekeza vitu hivyo.

"Nilikuwa nimesafiri kwenda Malaysia hivi karibuni. Nilipokwenda kwenye ofisi kwa lengo la kupata hati yangu ya kusafiria, nikaulizwa 'umetoka Tanzania kwenye nchi ya amani?' Hivyo, tutambue na kuilinda amani hii tuliyonayo," alisema.

**MALEZI**

Padri wa Kanisa Katoliki Parokia ya Maonano Mawela, Jimbo Katoliki la Moshi, mkoani Kilimanjaro, Deo Bahati, aliwataka Watanzania kuitumia sikukuu ya Krismasi kujikumbusha na kutimiza wajibu wa malezi kwa watoto badala ya kutegemea wengine kuwasaidia kulea.

Aliwataka wanafamilia kujinyenyekeza na kujiona bado ni watoto kwa wazazi wao hata kama wamekuwa wakubwa kiumri, wana fedha, mali, madaraka, taaluma au wamekuwa wafanyabiashara wakubwa.

"Nikipigwa vita popote pale nitakapokuwa, sehemu ya kwanza kukimbilia ni nyumbani, kwa sababu ndiko faraja ya kweli inakopatikana.

"Baba ukija nyumbani, uje kama baba wa familia, vivyo hivyo mama ukija nyumbani, uje kama mama wa familia. Usije kama daktari, mwalimu au mfanyabiashara," alionya Padri Bahati.

Pia aliwataka vijana pindi wanapokwenda majumbani mwao kwa ajili ya sikukuu au wakati mwingine wowote, waende kama watoto na kuacha vyeo na umaarufu wao kwa sababu wazazi wao hawakuzaa mfanyabiashara, daktari wala mwalimu, bali mtoto.

**KUABUDU MIZIMU**

Padri wa Kanisa la Katoliki la Kristo Mfufuka wilayani Tanga, Martine Kihiyo, aliwataka Wakristo kuacha tabia ya kujihusisha na shughuli za uganga wa kienyeji au kuabudu mizimu pindi wanapopatwa na matatizo katika maisha.

Akihubiri katika ibada ya sikukuu ya Krismasi jana, alisema kuwa baadhi ya Wakristo wanapokea sakramenti, lakini wanajishughulisha na uganga wa kienyeji na kuabudu mizimu chini ya miti na kumsahau Mungu.

Hivyo, aliwataka watu hao kujenga mazoea ya kupeleka matatizo na shida zao kwa Mungu na si kuabudu mizimu.

**UPENDO**

Askofu wa Jimbo Katoliki la Tanga, Mhashamu Thomas Kiangio, alisisitiza amani, upendo katika familia kwa Watanzania, akionya kuwa wasipoyaishi hayo, haitakuwa na maana kwa sababu upendo ukikosekana kunatokea mtafaruku.

Akihubiri wakati wa ibada ya sikukuu ya Krismasi katika Kanisa la Mtakatifu Antony wa Paduo jijini Tanga, alisema amani ni tunu kubwa ambayo imeachwa na waasisi wa nchi, hivyo lazima itunzwe na ienziwe.

Alisema pasipokuwa na amani na watu wenye upendo, jamii itafarakana kama inavyoshuhudiwa sasa katika mataifa mengi duniani.

**TAMAA**

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga, Mhashamu Liberatus Sangu, aliwataka watu wote duniani kuwa wanafamilia ya Mungu na kuacha kutenda dhambi na kutoendekeza tamaa za kidunia ambazo zinasababisha machafuko na amani kutoweka.

Alihubiri wakati wa mkesha wa Krismasi uliofanyika katika Kanisa Katoliki Parokia ya Ngokolo mjini Shinyanga, Askofu Sangu alisema dunia kwa sasa haina amani, kila siku mataifa yanapigana vita kwa sababu wanadamu wameingiwa na tamaa.

"Dunia sasa hivi haina amani, mataifa yanapiga vita kila kukicha, tunamhitaji Yesu azaliwe katika familia zetu, mioyoni mwetu, tufanye mapinduzi ili Kristo awe amani yetu, nje ya Yesu hakuna amani wala upendo ni vurugu tupu," alionya.

Aliwataka waumini wa kanisa hilo na wananchi kwa ujumla washerehekee sikukuu hizo na familia zao na kuepuka anasa ikiwamo ulevi uliopindukia.

**ISRAEL, PALESTINA**

Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Kanisa Katoliki Dar es Salaam, Juda Thadeus Ruwa'ichi, aliwataka Watanzania kuendelea kuombea amani ya Israel na Palestina, wanaokabiliwa na vita kati yao. Imeondoa utamaduni wa waumini kwenda kutembelea mji wa Bethlehem, alikozaliwa Yesu.

Pia aliwataka Watanzania kusherehekea sikukuu ya Krismasi kwa kuwa Yesu alikuja kwa ajili yao ili kuwapa hadhi ya kuwa watoto, kuwaokoa na kuwatetea.

Alisisitiza Watanzania kutafakari siku hiyo kama kweli Yesu ana nafasi katika mioyo yao, kazi zao, jumuiya na mapito yao.

**MWENDOKASI**

Naye Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Dodoma, Beatus Kinyaiya aliwataka madereva wa vyombo vya moto nchini kuacha kuendesha kwa mwendokasi ili kupunguza ajali za barabarani zinazosababisha vifo na ulemavu.

Alisema usafiri wa pikipiki, maarufu bodaboda, madereva wake wamekuwa wanaendesha bila kuzingatia sheria za usalama barabarani. Wanaongoza kwa kusababisha vifo na majeruhi nchini.

***Imeandaliwa na Godfrey Mushi (Moshi), Cynthia Mwilolezi, Daniel Sabuni (Arusha), Oscar Assenga (Tanga), Jaliwason Jasson (Mbulu), Nebart Msokwa (Mbeya), Idda Mushi (Moshi), Steven William (Muheza), Oscar Assenga (Tanga) Marco Maduhu (Shinyanga), Alphonce Kabilondo (Geita), Rahma Suleiman (Zanzibar), Beatrice Shayo (Dar) na Renatha Msungu (Dodoma).**



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akishiriki ibada ya Sikukuu ya Krismasi katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mwenyeheri Maria Theresa Ledochowska Kiwanja cha Ndege Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

## MJAMZITO ALIYEBAKWA

# Polisi wilayani Mkuranga wazua jambo

**Na Mwandishi Wetu aliyekuwa MKURANGA**

NI miezi saba sasa tangu tukio la mjamzito kubakwa na kufungwa katika kiroba wilayani Mkuranga, mkoani Pwani, Jeshi la Polisi halijachukua hatua.

Hata pikipiki iliyokamatwa eneo la tukio na kupelekwa Kituo cha Polisi Vikindu, nayo imeachiliwa na kuzua mjadala miongoni mwa wananchi.

Usiku wa Juni 5, mwaka huu, mama huyo, mkazi wa Mtaa wa Kazole, Kata ya Vikindu, wilayani Mkuranga, alibakwa na hatimaye kufungwa katika kiroba akiwa amepoteza fahamu.

Wiki sita baadaye, ujauzito wake uliothibitishwa hospitalini kuwa wa pacha uliharibika. Alijifungulia Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga - si riziki - Julai 12, mwaka huu.

Kifungu cha 131(1) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, kinaelekeza adhabu ya kifungo cha maisha gerezani kwa mtu anayetenda kosa la kubaka; adhabu ikiambatana na viboko 12 na faini ambayo itatamkwa na mahakama.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Kamishna Msaidizi Protas Mutayoba anasema, hadi Jumamosi iliyopita, Polisi walikuwa hawajakamata mtuhumiwa yeyote. Hivyo, kesi hiyo haijafikishwa mahakamani.

"Tumekuwa tunapata taarifa kutoka kwa mume wa mwathirika wa tukio hilo kwamba wazazi wa watuhumiwa wamekuwa wakifika nyumbani kwake, wakitaka suluhu ili kesi hiyo iishe.

"Kwa mujibu wa Ofisi ya Mpelelezi Mkuranga, mume wa mwathirika alielekezwa kufanya mtego kwa wazazi hao ambao aliwaambia waende kuomba radhi wakiwa na watoto wao waliofanya tukio hilo na siku hiyo polisi wapatiwe taarifa ili kuwakamata.

"Hata hivyo, njia hiyo haijazaa matunda kwani upande wa mlalamikaji mwezi mmoja uliopita (Novemba mwaka huu) walitoa taarifa kwa mpelelezi wa kesi hiyo kwamba wazazi wa vijana hao walikwenda tena nyumbani kwa mwathirika na kuendelea na ajenda ya kuomba wamalizane nje ya utaratibu wa kisheria," alisema.

Kamanda Mutayoba alieleza kuwa mpango wao wa kuwaandalia mtego wa kuwakamata watuhumiwa ulikwama kutokana na familia ya mlalamikaji kutowapa taarifa polisi. Ilitoa taarifa ya kutembelewa na wazazi wawili wa watuhumiwa baada ya wazazi hao kuondoka nyumbani kwa mlalamikaji.

Baadaye mwandishi alizungumza na mume wa mwathirika (jina tunalo). Akathibitisha wanawake wawili kufika nyumbani kwake kwa lengo la kuomba radhi kutokana na ukatili uliofanywa na watoto wao dhidi ya mkewe aliyekuwa mjamzito.



Ukatili uliofanywa dhidi ya mjamzito Juni 5, mwaka huu.

"Ni kweli mwezi uliopita (Novemba) walikuja hapa nyumbani kwangu kinamama wawili, mama yake Adam na mama wa Rajabu. Walituletea na chakula - kilo moja ya mchele. Wakasema kilichowaleta ni kuomba radhi kutokana na kile walichokifanya watoto wao dhidi ya mke wangu.

"Wakasema wako tayari kulipa chochote tulimalize hili suala kifamilia badala ya kulifikisha mahakamani. Mimi niliwaambia waje na hao vijana wao ili wanieleze kwanza sababu ya kufanya ukatili huo dhidi ya mke wangu; maana tuliishi nao vizuri tu katika nyumba moja.

"Walipotoka ndipo nikakumbuka nina namba za mpelelezi wa kesi hii. Nikampigia na kumweleza kilichotokea, akasema tuwawekee mtego ili wakamatwe; lakini hawajarejea tena hapa nyumbani," alisema.

Alibainisha kuwa anajua anwani za wazazi hao wa watuhumiwa. Mmoja anaishi Mbande, wilayani Temeke na mwingine anaishi Kitongoji cha Magomeni, Kata ya Vikindu, wilayani Mkuranga.

Kuhusu pikipiki iliyokuwa inashikiliwa katika Kituo cha Polisi Vikindu ikihusishwa na tukio hilo, Kamanda Mutayoba alisema:

"Pikipiki ilikamatwa kama kielelezo cha watuhumiwa. Polisi waliiachia huru kwa mmiliki ambaye alifika kituoni na vielelezo vya umiliki na kudai kwamba alikuwa amemwazimisha kwa muda mtuhumiwa aliyeitelekeza eneo la tukio."

### UFAFANUZI WIZARANI

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Dk. Gunini Kamba, aliunda timu ya kufuatilia namna matabibu wa Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga walivyotoa matibabu kwa mjamzito huyo.

Hata hivyo, mwandishi alipohitaji ufafanuzi kuhusu uchunguzi huo, Dk. Kamba alisema suala hilo haliko mikononi mwake kutokana na uzito wake. Akaongeza kuwa linashughulikiwa na Wizara ya Afya.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, akitoa ufafanuzi kwa mwandishi kuhusu suala hilo, alisema matabibu walikiuka miongozo ya kutoa matibabu kwa wajawazito.

Naibu Waziri huyo ambaye kitaaluma ni daktari wa binadamu, alisema mwongozo unaelekeza muda wa pacha kupishana kuzaliwa haupaswi kuzidi dakika 30.

"Mtoto wa kwanza akishazaliwa, mwingine anapaswa kuwa ametoka tumboni ndani ya nusu saa (dakika 30). Kama hajazaliwa ndani ya muda huo, upasuaji unapaswa kufanyika.

"Kwahiyo, watendaji wetu wa Mkuranga hawakuzingatia mwongozo, ndio maana tumechukua hatua," alisema Dk. Mollel ambaye hakuwa tayari kuweka wazi hatua zilizochukuliwa dhidi ya watendaji hao.

### TUME YA HAKI

Mkuu wa Kitengo cha Sheria Tawi la Dar es Salaam la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Philemon Mponezya, analinyooshea kidole Jeshi la Polisi kwa kuchelewa kuchukua hatua.

Mponezya anasema: 'Kilichotendwa dhidi ya mjamzito ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria za nchi. Ubakaji ni kosa la jinai na lina utaratibu wake wa kushughulikiwa kwa maana vyombo vya kijinai, likiwamo Jeshi la Polisi lenye jukumu la kukamata, kupeleleza na kuwafikisha wahusika mahakamani.

"Sisi (tume) pia tunaweza kuingia kuchunguza haki za binadamu kwa sababu ule ni unyanyasaji na utesaji wa mwanamke. Kumbaka mwanamke, tena mjamzito, ni udhalilishaji na utesaji.

"Mamlaka husika za kijinai zinatakiwa zichukue hatua haraka sana kwa sababu kama ni tangu mwezi wa sita (Juni) mpaka sasa, kuna ucheleweshwaji mkubwa. Hao wabakaji walipaswa kuwa wameshafikishwa mahakamani.

"Kuchelewa kuwafikisha mahakamani kunatengeneza hatari ya watuhumiwa kuharibu upelelezi. Wakamatwe na kufikishwa mahakamani ili kesi yao isikilizwe na haki ipatikane.

"Kutochukua hatua ni kuliaibisha Jeshi la Polisi, lionekane halifanyi kazi kwa wakati. Pia ni kumkarahisha yule mwathirika kuona kwamba serikali haifanyi kitu chochote."



Maziko ya watoto pacha waliozaliwa wakiwa si riziki, yakifanyika katika eneo la msikiti ulioko karibu na Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani Julai 12, mwaka huu. **PICHA ZOTE: MPIGAPIGA WETU**

# KRISMASI PICHANI



Waumini wa Parokia ya Mtakatifu Petro Oysterbay jijini Dar es Salaam, wakiwa kwenye ibada ya Krismasi jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Padri wa Kituo cha Don Bosco Oysterbay, Luka Mulayinkal (kulia), akitoa sakramenti ya ubatizo kwa mtoto Godwin Kassian aliyeshikwa na baba wa kiroho Thomas Simon, katika ibada ya ubatizo iliyofanyika kigango cha Mtakatifu Paulo wa Msalaba Mikocheni A, Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya kusherehekea sikukuu ya Krismasi. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Wananchi wakiwa kwenye foleni kusubiri huduma ya nyama, kilo moja iliuzwa kwa 11,000/- ikiwa ni ongezeko la shilingi 3,000 katika eneo la Goba Tegeta A, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Paroko wa Parokia ya Mtakatifu Petro Oysterbay, Padri Alistair Makubi, akiongoza ibada ya mkesha wa Krismasi juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Waumini wa Kanisa la Romani Katoliki la Kristo Mfufuka lililoko Mtaa wa Majengo Shimoni, wilayani Muheza, Tanga, wakitoka katika ibada ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo iliyoongozwa na Padri Martine Kihiyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Kwaya ya Kanani ya Kanisa Kuu la KKKT Dayosisi ya Dodoma ikiimba kwenye ibada ya Krismasi iliyofanyika Kanisa la Usharika wa Dodoma mjini jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII




# Kiwanda cha kusarifu dagaa kilete tija kiuchumi Zanzibar

**MAMILIONI** ya fedha yanatarajiwa kuiinua kiuchumi Zanzibar baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa kinachoendelea kujengwa Kama, Wilaya ya Magharib A Unguja, chenye uwezo wa kuzalisha tani 20 kwa siku.

Kiwanda hicho kitakapokamilika kitakuwa cha aina yake katika ukanda wa pwani wa Afrika Mashariki.

Dagaa ni moja wapo ya mazao makuu ya kimkakati visiwani humo katika sekta ya uvuvi na mazao ya baharini na kuliinua zao hilo kupitia ushindani wa kisasa kwa ubora katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Uzalishaji wa dagaa Zanzibar umekua kutoka tani 2,405 zenye thamani ya Sh. bilioni 10.33 hadi 21,827 zenye thamani ya Sh. bilioni 89.31.

Mafanikio ya sekta ya dagaa yamechochea kuongezeka kwa uzalishaji wa jumla wa sekta ya uvuvi wa samaki kutoka tani 38,107 kwa mwaka 2020 hadi 80,085 zenye thamani ya Sh. bilioni 569.08 kwa mwaka huu.

Mchango wa sekta ya uvuvi katika uchumi wa buluu umeongezeka kufikia wastani wa asilima 17.40 ambayo ni mafanikio makubwa na uwapo wa kiwanda cha kukausha dagaa utakaochochea zaidi ongezeko la kipato cha uchakataji wa samaki kutoka wastani wa sasa wa Sh. 435,300 na kuongeza kipato cha wajasiriamali wa samaki kutoka wastani wa sasa wa Sh. 742,500.

Kiwanda hicho kitakapomalizika kitaongeza ajira kwa wananchi na takwimu za sasa zinaonesha asilimia 21 ya ajira za wananchi wote wa Zanzibar zinatokana na sekta zote za uchumi wa buluu na sensa ya mwisho ya uvuvi ya mwaka 2020 Zanzibar inawavuvi 88,000.

Mradi huo wa kujenga miundombinu ya dagaa ni miongoni mwa utekelezaji wa ahadi ya Rais Dk. Mwinyi ambaye aliwaahidi wananchi wajasiriamali wa usarifu wa dagaa.

Zanzibar ina wastani wa wajasiriamali 16,000 wa dagaa, Unguja ni 14,000 na 12,000 Pemba na jumla maeneo matatu yametengwa kwa ajili ya mradi wa usarifu wa dagaa ikiwamo Kama, Fungu refu na Ndagoni.

Mradi huu unatarajia kutumia Sh. milioni 23 ambazo zimejumuisha ujenzi wa viwanda viwili vya kusarifu dagaa, majengo ya kuoshea dagaa ya kuchemshia, jengo la mtambo baridi kwa ajili ya kuhifadhia na mtambo wa kuzalisha barafu na jengo la biashara.

Zanzibar ina utajiri mkubwa wa uvuvi na bahari ikitumiwa vizuri italeta maendeleo makubwa kupitia fursa zilizomo baharini na ukanda wa pwani.

Uvuvi ni muhimu kwa maendeleo ya jamii katika nchi na ili sekta ya uvuvi ilete tija hakuna budi kutumia teknolojia za kisasa na ushirikishwaji wa sekta binafsi, ndio maana serikali inahamasisha wananchi kuendelea na uvuvi endelevu usioharibu mazingira ya bahari.

Takwimu zinaonesha kuwa wananchi wa Zanzibar wanatumia samaki kwa wastani wa kilo 22 kwa mtu mmoja kwa mwaka, kiasi hicho ni kikubwa kulinganisha na wastani wa matumizi ya kiwango cha dunia ambacho ni kilo 20.5 kwa mtu mmoja kwa mwaka.

Wananchi wanashauriwa kuongeza kiwango cha matumizi ya chakula kinachozalishwa baharini ikiwamo dagaa kwa kuimarisha afya ya lishe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kwa heri 2023 uliboresha elimu

**MWAKA** 2023 ambao unaelekea ukingoni, ulikuwa ni wa mchakato wa mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na Mabadiliko ya Mitaala na kukamilika na kuwasilishwa katika ngazi ya uamuzi.

Lakini kulikuwa na sintofahamu kutokana na baadhi ya wadau kuuliza kuhusu elimu ya msingi kuishia darasa la sita kutokana na kuwapo taarifa kwamba utaratibu huo ungeanza mwaka ujao.

Kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda ni kwamba utaratibu wa elimu ya msingi kuishia darasa sita utawakuta wale ambao hawajaanza shule.

Waziri anasema, darasa la saba bado lipo, uamuzi utakapofanyika, itachukua muda kidogo kuingia elimu ya msingi ya darasa la sita, kwa kuwa mapendekezo yaliyopo ni kuwa mitaala mipya.

Profesa Mkenda anasema, Sera ya Elimu inataka kutekelezwa kwa pendekezo lililotoka mwaka 2014 kwamba elimu, ya msingi iwe miaka sita na elimu ya lazima iwe miaka 10.

Mwanzoni mwa mwezi uliopita, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alitoa taarifa kuhusu maboresho hayo kwamba utekelezaji wake utaanza mwaka 2027 sambamba na kufuta mtihani wa darasa la saba.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu ni kwamba, badala yake kutakuwa kunafanyika tathmini darasa la sita, kwa ajili ya wanafunzi kujiunga na elimu ya sekondari ambayo itakuwa ni ya lazima.

Ni wakati wa ufafanuzi kuhusu kuidhinishwa kwa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na Mitaala ya Elimu Ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu katika kipindi cha maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu bungeni jijini Dodoma.

Uamuzi huo umefikiwa baada ya kubainika kwa changamoto mbalimbali zikiwamo, mfumo wa elimu kujikita zaidi kwenye elimu ya jumla na kukosa fursa za elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji na njia mbalimbali za ujifunzaji kutokidhi kulingana na mazingira.

Baadhi ya changamoto hizo ni mitaala kutokidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia, mfumo usio na ufanisi wa udhibiti na ithibati ya elimu na upungufu wa nguvu kazi.

Changamoto hizo ndizo zinaelezwa kuwa zilizaa hitaji la kuboresha sera ya elimu, ili kukidhi mahitaji ya sasa na wakati ujao, huku maeneo yaliyoboreshwa yakiwekwa hadharani.

Maeneo hayo ni Sera ya Elimu na Mafunzo kufanyiwa mabadiliko kwenye maeneo kadhaa ikilinganishwa na sera iliyopita kwa kuongeza fursa za elimu ya amali (elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi) ambayo itaanza kutolewa kuanzia kidato cha kwanza.

Aidha, mwaka 2023 umekuwa ni wa kutangazwa kuanza kutolewa kwa elimu ya ualimu kwa wahitimu waliomaliza kidato cha sita na kuendelea, huku mafunzo ya ualimu yakijumuisha mwaka mmoja wa mafunzo chini ya uangalizi baada ya kuhitimu mafunzo tarajali.

Lakini kutakuwa na mfumo wa upimaji na tathmini ambao utazingatia umahiri unaohitajika kwa kila ngazi, kwa lengo la kuwa na upimaji endelevu na matumizi ya mbinu mbalimbali za upimaji na tathmini ya maendeleo ya wanafunzi katika kujifunza.

Wakati hayo yakiendelea, serikali pia itasimamia matumizi ya kitabu kimoja cha kiada kwa kila somo katika elimu ya msingi na Sekondari, ili kufanikisha upimaji wa matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji unaofanana.

Katika mfululizo huo, serikali itaweka utaratibu wa kubaini na kuendeleza wanafunzi wenye vipaji na vipawa mbalimbali, ili viweze kuwanufaisha kwanza kisha jamii na taifa kwa ujumla.

HABARI KITAIFA

## HST yaibuka na kampeni maalum visiwani Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

CHAMA cha Himofilia Tanzania (HST) kimezindua kampeni visiwani Zanzibar iliyolenga kuinua ufahamu wa ugonjwa huo kwa viwango vipya ili kuwafikia Watanzania wengi zaidi wenye changamoto hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Katibu wa chama hicho, Dk. Abdallah Makalla, alisema kampeni hiyo itafanyika kupitia matukio mbalimbali ikiwamo mikutano na waandishi wa habari, ushirikiano wa afya na elimu kwa umma.

Alisema lengo ni kuvunja vizuizi, kuondoa dhana potofu na kuangazia hali halisi ya kuishi na himofilia na kwamba kampeni hiyo inafanyika chini ya kaulimbiu ya 'Uvujaji damu, ulemavu na vifo vitokanavyo na himofilia sasa basi'.

"HST imeendelea kuwa imara katika dhamira yake ya kubadilisha simulizi za himofilia nchini na kwingineko. Kwa usaidizi unaoendelea na ushirikiano, tunajitahidi kuelekea ulimwengu ambao himofilia haizuii tena uwezo, badala yake ni hali inayofikiwa kwa uelewa, huruma na utunzaji bora," alisema.

Katibu huyo alisema takwimu zinaonesha katika kila watu 100,000 ulimwenguni, mmoja ana ugonjwa wa himofilia. Kwa Tanzania, kuna zaidi ya wagonjwa 6,000 huku asilimia 97 ya wagonjwa wa himofilia hawajui kama wana tatizo hili.

Dk. Makalla alisema kuwa hadi sasa ni sehemu ndogo tu ya wagonjwa waliotambulika na ambao wanapokea matibabu.

Alisema HST inaamini kuwa changamoto hiyo inachangiwa na ukosefu wa elimu kwenye jamii na wataalamu wa afya juu ya himofilia na magonjwa ya uvujaji damu na imani potofu juu ya ugonjwa huo.

Alibainisha kuna changamoto ya upatikanaji vipimo vinavyoweza kutambua ugonjwa huo, ufikiaji mdogo wa huduma ya afya na gharama kubwa za matibabu. Ni vikwazo vinavyochangia kutogundulika mapema kwa wagonjwa wa himofilia.

"Ulimwenguni himofilia inasalia kuwa tatizo kubwa la kiafya lenye viwango tofauti vya ukali na uhitaji wa usimamizi wa maisha yote.

"Nchini changamoto hizi zinachangiwa na hali duni ya kimaisha na ukosefu wa uelewa kwa jamii na wataalamu wa afya," alifafanua.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu huyo, HST ina dhamira ya kueneza uelewa kwa jamii na kwa wataalamu wa afya kwa njia ya mafunzo kwenye vyombo vya habari, nyumba za ibada na namna mbalimbali ili kusaidia utambuzi wa mapema wa wagonjwa wa himofilia na upatikanaji matibabu ya mapema ili kupunguza vifo na ulemavu unaotokana na himofilia.

Chama hicho kilianzishwa mwaka 2009 na kimekuwa mwanga wa matumaini katika vita dhidi ya himofilia, kikijitolea kuboresha huduma na usaidizi kwa watu wenye ugonjwa huo na matatizo yanayosababishwa na kuvuja damu.




Diwani wa Kata ya Majengo, wilayani Muheza, Tanga, Mukadam Sabuni, akipanga utaratibu wa kugawa zawadi ya vyakula kwa wananchi vilivyotolewa msaada na Taasisi ya Silver Crescent juzi kutoka nchini Uturuki, wananchi 240 wilayani humo walipata msaada huo pamoja fedha. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wabaini wagonjwa wanaohitaji upasuaji macho kuepuka upofu

**Na Mwandishi Wetu,** BAGAMOYO

WILAYA ya Bagamoyo, mkoani Pwani imegundua wagonjwa wapya wa macho 30 wanaohitaji upasuaji wa haraka ili kuwaepusha na upofu kati ya 500 waliojiandikisha kufanyiwa uchunguzi wa macho Desemba 21 na 22 mwaka huu.

Mwezi Oktoba mwaka huu, katika kambi nyingine ya uchunguzi huo, madaktari bingwa waliwachunguza wagonjwa 1,200 wenye matatizo ya macho wilayani Bagamoyo.

Dk. Jane Mcharo ambaye ni Mratibu wa Huduma za Macho wa Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo, akizungumza katika uzinduzi wa kambi ya uchunguzi wa macho iliyofadhiliwa na Taasisi ya Al Atar A' Charitable Foundation (ACF), alisema tatizo hilo ni kubwa kwa sasa wilayani mwake.

"Tatizo la macho ni kubwa Bagamoyo. Mwezi wa Oktoba tulikuwa na kambi nyingine kama hii.

Tuliwaona na kuwachunguza wagonjwa 1,200 wenye matatizo ya macho.

"Unaweza kuona ukubwa wa tatizo na kwa kambi hii mpya ya Desemba mpaka kufikia jana, tumewaona wateja 200 na wateja 30 tayari wamefanyiwa upasuaji.

"Wengine wamepata miwani, dawa na ushauri wa kitaalamu na kurejea majumbani. Kwa hiyo, ni tatizo kubwa, tunahitaji sana hawa wadau kufanya hizi kambi za mara kwa mara ili kuimarisha afya za wananchi wa Wilaya ya Bagamoyo, afya na maendeleo vinakwenda pamoja, kama hakuna afya hakuna maendeleo," alisema.

Magonjwa tishio ya macho yanayosababisha upofu ni vikope (trakoma), mtoto wa jicho (cataract) na presha ya macho.

Akizungumzia ufadhili wao, Ofisa Uhusiano na Mratibu wa Kambi za Macho wa Taasisi ya Al Atar A' Charitable Foundation, Abubakari Mwinyimbegu, alisema katika kambi hiyo wamefadhili shughuli za uchunguzi wa macho, upasuaji wa macho na utoaji wa miwani tiba.

"Tuko hapa Bagamoyo kwa ajili ya kuwaona watu 500 pamoja na kuwapa miwani watu 150 na kufanya upasuaji kwa watu 50.

"Mwezi Oktoba kulifanyika uchunguzi na wakagundua kuna watu wanatakiwa kufanyiwa operesheni, lakini hawakuweza kuwafanyia. Kwa hiyo, sisi tumekuja tufanye uchunguzi, kwa wale ambao hawakufanyiwa kipindi hicho.

"Lengo na madhumuni, kila mtu huduma hii imfikie na aweze kunufaika kwa huu msaada ambao sisi tunautoa. Asilimia 90 ya wananchi wanajitokeza na kupokea misaada hii kwa moyo na mikono miwili," alisema.

Kabla ya ufunguzi huo, Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Rehema Kingu, aliishukuru Taasisi ya Al Atar A' Charitable Foundation (ACF) kwa kwenda Bagamoyo kutoa huduma kwa wananchi bila malipo.

Alisema huduma ambazo zinatolewa ni pamoja na kupima macho, kufanyiwa upasuaji wa macho na kutoa dawa bila malipo.

Mmoja wa wagonjwa waliopata huduma hiyo, Rehema Mzee, alisema kuwa kabla ya kufanyiwa uchunguzi na baadaye upasuaji, macho yake yalikuwa hayaoni vizuri, alikuwa hawezi kusoma kwa mbali na alikuwa hawezi kusoma maandishi madogo, lakini hivi sasa anashukuru amepata tiba.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**





Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, mkoani Singida, Kemirembe Lwota (kushoto), akipewa maelezo na Mhandisi Umwagiliaji mkoani humo, Japhet Senyina, alipotembelea juzi miradi ya umwagiliaji ya Msemembo, Saranda, Chikuyu na Udimaa iliyopo katika wilaya hiyo kujua changamoto zilizoko na kuangalia namna ya kuzitafutia ufumbuzi. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

## BEI MPYA MATIBABU

# Wamiliki hospitali binafsi watishia kutopokea wenye bima za NHIF

**Na Joseph Mwendapole**

WAMILIKI wa hospitali binafsi nchini wametishia kugomea kutibu wagonjwa wanaohudumiwa kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) iwapo bei mpya zilizotangazwa na mfuko huo zitaanza kutumika Januari Mosi mwakani kama ilivyopangwa.

Kupitia taarifa yao kwa vyombo vya habari jana, wamiliki hao wanadai kitita kipya kilipitishwa na serikali bila kuwashirikisha, kitasababisha hospitali nyingi kufungwa kutokana na kupata hasara kikianza kutumika.

"Kwa miaka saba sasa tangu gharama mpya zitangazwe, hazikuwahi kuboreshwa na ilikuwa matarajio yetu kwamba NHIF itatangaza ongezeko la gharama za huduma na si kupunguza.

"Kwa kuzingatia ukweli huu pamoja na mengine kama ucheleweshaji malipo kwa zaidi ya miezi minne, mfumuko wa bei, kushuka kwa thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani kwa zaidi ya asilimia 20 ndani ya miaka saba APHFTA (chama chao) tumeona tutashindwa kuwahudumia wanachama wa NHIF kama bei hizi zitaanza kutumika rasmi," wanafafanua kupitia taarifa yao hiyo.

Wanatoa mfano kuwa kushuka gharama za kumwona daktari, upasuaji na kuchuja damu (dialysis), kutawafanya washindwe kumudu gharama halisi za kuhudumia wagonjwa wanaotibiwa kwao.

Kupitia taarifa yao hiyo, wanadai bei za mwisho ziliwekwa tangu mwaka 2016 na tangu wakati huo hakujawahi kufanywa mapitio licha ya gharama za maisha kupanda. Kushusha gharama za matibabu ni sawa na kuzichimbia kaburi hospitali binafsi.

"Malipo yenyewe kwa watoa huduma yanaweza kukaa miezi hata sita hayajalipwa na wakati mwingine wanakataa baadhi ya madai ya malipo bila sababu za msingi. Sasa haya yote hayajatatuliwa wanakuja kushusha gharama, si wanataka kutuua!" inaelezwa katika taarifa hiyo.

Taarifa hiyo inasema NHIF iliwaambia wafunge mfumo wa mtandao kwa ajili ya kuwasilisha madai yao ya huduma wanazotoa ili wawe wanalipwa ndani ya siku 14 baada ya kuwasilisha madai hayo, lakini hali ni ile ile tangu wafunge mfumo huo.

"Tumefunga mfumo ambao umetugharimu fedha nyingi, lakini hizo siku 14 walizosema hawalipi na bado tunalazimika kusubiri miezi minne hadi sita, kama wanaona gharama za uendeshaji zimekuwa kubwa, wapunguze matumizi yao yasiyo ya lazima lakini watibu watu.

"Kwenye hili tunamwomba Rais Samia Suluhu Hassan atusaidie kwa sababu kwa hiki kitita ni kama wanataka kuzifunga hospitali binafsi.

Rais wetu siku zote amekuwa akisisitiza ushirikishwaji wa sekta binafsi kupitia PPP lakini hawa ni kama hawataki kuona tunaendelea kuwapo," inasisitizwa katika taarifa hiyo.

Wanasema APHFTA iliwasilisha mapendekezo ya namna ya kuboresha uhai wa mfuko ikiwamo kuitaka NHIF ipitie upya mapendekezo ya kibiashara kwa bidhaa zake vikiwamo vifurushi vya WEKEZA, TIMIZA, NAJALI na vinginevyo.

Inaelezwa katika taarifa hiyo kuwa walipendekeza NHIF itumie mfumo wa ukusanyaji madeni wenye ufanisi zaidi na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) ina maelezo ya kiasi kikubwa cha fedha ambacho hakikusanywi na NHIF kwa taasisi nyingi.

"Kabla ya kutafuta suluhisho la nje, NHIF inapaswa kuonesha msimamo wa kupunguza gharama za uendeshaji ndani ya mfuko na tukumbuke kwamba vituo vya afya, hospitali na NHIF wanategemeana kwa ajili ya kuishi na kuwa endelevu, hivyo hatupaswi kudhoofishana," wanaeleza katika taarifa yao hiyo.

Wanasema kikao cha APHFTA kilibaini kuwa baada ya ukaguzi wa madai ya Septemba, Oktoba na Novemba mwaka huu, vituo vyote binafsi kuanzia ngazi ya dispensari mpaka hospitali za rufani zingepata hasara ya wastani wa asilimia 25.

"Na hii ni bila kuzingatia makato ya kila mwezi ukizingatia makato hayo yenye wastani wa asilimia 10 ambayo makato yenyewe yamejaa sintofahamu na utata mwingi yanafanya jumla ya hasara kufikia asilimia 35 kwa hospitali binafsi," walifafanua katika taarifa hiyo.

Akizungumzia madai hayo, Meneja Mawasiliano wa NHIF, Angela Mziray alisema suala la malipo ni mchakato mrefu kujiridhisha kama madai ya mhusika ni halali na kama kuna mambo hayajakaa sawa basi madai yanarejeshwa kwa mhusika ili kufanya marekebisho.

"Kwa utaratibu wetu NHIF madai ambayo yamenyooka mhusika anapaswa kulipwa ndani ya siku 60, lakini mleta madai akileta huwezi kulipa tu bila kujiridhisha, lazima ujiridhishe kabla ya kulipa.

"Kwahiyo, wakati mwingine kunakuwa na mashauriano na mleta madai. Hapo ndipo muda unaweza kutumika mwingi," alisema Angela.

Kuhusu ushirikishwaji wa wadau wa sekta binafsi katika kuandaa vitita vipya, Angela alisema NHIF ina ushahidi wa namna ilivyokaa na wadau mbalimbali wakiwamo APHFTA na kupata maoni yao wakati wote wa mchakato wa bei mpya.

"Tatizo hapa ni kwamba unapomshirikisha mtu anadhani kila anachosema yeye ukichukue, kitu ambacho hakiwezekani.

"Hizi bei mpaka zinatoka, zimepitia mchakato wa miaka miwili. Inawezekana ikawa ajenda ya mtu mmoja au wawili wakataka kuifanya ajenda ya chama.

"Kwa hiyo kama ni kuchelewesha malipo haiwezekani kwamba wote wanacheleweshewa malipo. Kama kuna mtu mmoja awasilishe malalamiko yake kwa mfuko yafanyiwe kazi badala ya kuzungumza kana kwamba ni suala la nchi nzima," alisema.

# DC, AG waitwa mahakamani mgogoro jengo EAGT

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masijala ya Mwanza imewaita mahakamani Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, wanaolalamikiwa kwenye mgogoro wa jengo kati ya Kanisa la Evangelistic Assemblies of God of Tanzania (EAGT) na Kanisa la Assemblies of God Gospel Church International (AGGCI).

Mahakama hiyo ilifikia uamuzi huo mbele ya Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza, Stanley Kamana baada ya mwombaji katika shauri hilo, Mchungaji Benson Kitonka, kuomba amri hiyo kutokana na mjibu maombi wa kwanza DC Makilagi kutoa amri Desemba mosi, mwaka huu.

Makilagi aliamuru mwombaji atolewe nje ya jengo la kanisa lililopo Bugando na eneo lake lote na badala yake apelekwe kwa mdhamini aliyesajiliwa wa makanisa ya Evangelistic Assemblies of God of Tanzania.

Mahakama iliamuru hali ilivyo kwa jengo la Kanisa la Bugando lililopo kwenye kiwanja namba 50 block 2 Bugando Kaskazini, Manispaa ya Nyamagana na mpango yote yatunzwe hadi maombi yatakaposikilizwa.

"Hali itabakia ilivyo bila kujali barua iliyotolewa na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana yenye kumbukumbu namba CAB.44/221/02/13 ya Desemba mosi mwaka huu," alisema.

Aliamuru pande zote mbili zinazohusika katika shauri hilo kufika mahakamani Februari 6, mwakani.

Mwombaji katika shauri hilo ni Mchungaji Benson Kitonka dhidi ya wajibu maombi DC Makilagi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Desemba mosi, mwaka huu DC Makilagi alimwandikia barua Mchungaji Benson kwamba Kamati ya Usalama ya Wilaya baada ya kupitia na kujadili mvutano unaoashiria uvunjifu wa amani ilibaini Kanisa la AGGCI halijasajiliwa, halijaruhusiwa kuanzisha matawi zaidi ya Kanisa la Makao Makuu Dodoma.

Pia barua hiyo ilisema kutokana na Askofu Moses Kuloka kuzikwa katika eneo hilo la kanisa ni busara jengo hilo likabaki kutumiwa na Kanisa la EAGT.



## Mimea vamizi Manyara, Arusha yapatiwa dawa

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MIMEA vamizi na tishio kwa uhai na ustawi wa mifugo, iliyokuwa imeota yenyewe kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 7,000 zilizoko nyanda za malisho za mikoa ya Manyara na Arusha, imeangamizwa.

Mkurugenzi wa Shirika la Tanzania People and Wildlife (TPW), Neovitus Sianga, alisema juzi kuwa wamekuwa wakiwawezesha wananchi wa maeneo hayo kielimu na motisha ili kupambana na mimea hiyo.

Sianga, alieleza mafanikio hayo, alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha wadau kilichokutanisha wizara mbalimbali, wataalamu wa mikoa na halmashauri, wenyeviti wa vijiji na viongozi wa kimila.

Alisema lengo la kikao hicho ni kujadili usimamizi wa nyanda za malisho na kutengeneza mikakati ya pamoja ambayo wataipeleka kwenye kikao kikubwa kwa ngazi za juu.

"Tumepanga mkakati thabiti wa usimamizi wa nyanda za malisho katika maeneo yetu ili kulinda maeneo yaliyotengwa," alisema Sianga.

Mkurugenzi huyo wa TPW, alisema moja kati ya jukumu muhimu ni kuboresha kamati za wafugaji ili zisimamie nyanda za malisho na tunawajengea uwezo na kuwasaidia kusimamia sheria ndogo ambazo wamejiwekea kulinda malisho.

Katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Malaigwanani wa Wilaya ya Monduli, Simon Melau, alisema wanajiwekea sheria ndogo ili kulinda eneo la malisho.

Naye Ofisa Nyanda za Malisho wa Wilaya ya Simanjiro, Dastan Mudolwa, alisema wana eneo la malisho hekta milioni moja katika vijiji 29.

Mudolwa, alisema pia wana mkakati wa kuunda kamati za nyanda za malisho katika vijiji hivyo ili waendelee kulinda malisho yao na kuendeleza harakati za kuyang'oa magugu vamizi.

Awali Katibu Tawala Msaidizi, anayeshughulikia uchumi na uzalishaji mali wa Mkoa wa Arusha, Hargeney Chitukuro, alisema wamekubaliana kuzipa jukumu kamati za nyanda za malisho kulinda na kusimamia maeneo hayo.

# Waziri awatupia lawama watendaji ukosefu wa dawa vituo vya afya

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema maeneo ambayo wananchi wake wanalalamikia kukosekana kwa dawa katika vituo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya ya mikoa, wakulaumiwa ni watendaji si serikali.

Akizungumza jana na wananchi wa Kata ya Pongwe katika Halmashauri ya Jiji la Tanga, alikokwenda kuzindua Zahanati mpya ya Kisimatui, Ummy alisema Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa na utaratibu mzuri wa kutoa fedha za ununuzi wa dawa nchini kote kwa asilimia 100.

"Katika kuhakikisha huduma ya afya inakuwa ya uhakika kwa wananchi, Rais wetu (Samia), anatoa fedha za dawa kwa asilimia 100, na ikitokea mahali hakuna dawa, sio kosa lake bali ni la watendaji," alisema. Alisema changamoto nyingine inayoikabili sekta ya afya ni ukosefu wa wahudumu kwa kuwa takwimu zinaonyesha ina upungufu kwa asilimia 60, lakini kupitia ajira zilizotolewa mwaka huu na Rais, Wizara itahakikisha kati ya wahudumu waliopata ajira hizo wanapelekwa Mkoa wa Tanga.

"Maelekezo yangu kwako Mkurugenzi, hata Kisimatui nako kuna watu na ni Watanzania, isije watumishi wakabaki mjini wakagona kuja Kisimatui, ni lazima tufanye mgawanyo, kwa hiyo tunataka kuona idadi ya watumishi wakiletwa hapa.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, serikali inatarajia kuwa Zahanati ya Kisimatui, ambayo itakuwa chachu kwa wananchi wa mtaa huo na majirani zao, ambao walikuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma za afya katikati ya Jiji la Tanga.

Ummy ambaye ni Mbunge wa Tanga, alisema serikali kupitia wizara yake imejitahidi kuhakikisha inasogeza huduma hiyo karibu na wananchi ili kuhakikisha wanaipata kwa wakati.

"Zahanati siyo majengo, tunachotaka kuona ni huduma bora za afya. Sisi wanasiasa tumemaliza wajibu wetu, sasa kazi kwenu watendaji, siyo kinamama wajawazito wanakuja hapa hawapati huduma," alisema. ...Kata ya Pongwe, ina watu 23,000 halafu ina kituo kimoja tuu cha afya na ndiyo maana tukaanza hii zahanati, lakini pia tutaangalia eneo jingine lenye watu wengi ili hizi huduma watu wazipate kwenye zahanati."

Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Erica Njana, alisema mradi huo umeigharimu serikali Sh. milioni 155, kwa ajili ya majengo ya huduma za nje na jengo la mama na mtoto.

"Halmashauri imetupatia dawa na vifaa tiba, vyenye thamani ya shilingi milioni 15 na matundu ya vyoo manne," alisema.



Katibu wa Chama cha Wachimbaji mkoani Manyara (MAREMA), Tawi la Mirerani, Rachel Njau (kushoto), akitoa taarifa ya chama hicho kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa wachimbaji madini ya Tanzanite uliofanyika juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wadau wataja vikwazo vya utatuzi migogoro ya familia

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WADAU wanaotekeleza mradi wa majaribio ya utatuzi na usuluhishi wa migogoro ya kifamilia nje ya vyombo vya Mahakama na Polisi (ADR) Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wamesema kinachowarudisha nyuma katika utekelezaji wa majukumu yao ni vyombo vingi vya ADR kukosa nguvu ya kisheria ya kutoa wito wa lazima.

Akizungumza juzi katika kikao cha kufunga mradi huo wa mwaka mmoja, Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Muhusin Kirua, alisema ADR kukosa mamlaka hayo kunawafanya baadhi ya watu kupuuza wanapoitwa kwenye usuluhishi.

Walishauri vikwazo hivyo kutazamwa na kufanyiwa marekebisho katika mradi ujao ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao na kuhakikisha wanatatua migogoro hiyo.

"Mtu mwingine anapokuwa amepewa wito, kwamba tunaomba uje leo tufanye utatuzi wa mgogoro wa kifamilia anapuuza. Lakini kuna tatizo pia la kutoheshimu uamuzi au maridhiano yaliyofikiwa, baada ya kufanya maridhiano.

Kiongozi wa kundi la wasaidizi wa kisheria, linalotekeleza mradi huo, Justine Laswai ambaye ameeleza namna wanavyoridhishwa na mafanikio makubwa ya utatuzi wa migogoro kupitia njia hiyo.


Laswai alisema: "Hii ni kwa sababu, ADR imetusaidia kupata njia fupi ya utatuzi wa migogoro. Kwanza haiachi malumbano ya kifamilia na inasaidia kuacha amani.

Alisema jamii imeipenda njia hiyo na kuipokea vizuri kama mkombozi wa migogoro kwenye jamii nzima kwa kuwa wanufaika wamepata haki zao bila gharama na pia uelewa juu ya huduma hii umekuwa mpana. Mradi huo wa mwaka mmoja, unaendeshwa na Shirika la KWIECO, kwa ufadhili wa Shirika la Legal Service Facility Tanzania (LSF).

Kabla ya kufunga mradi huo, Mratibu wa KWIECO/ADR, Lilian Mandari, alisema lengo kuu la mradi huo lilikuwa ni kuchangia utatuzi wa migogoro ya kifamilia kwa kutumia njia mbadala ya utatuzi wa migogoro kwa ufanisi na kupunguza mashauri yanayoweza kutatuliwa kwenye jamii.

Pamoja na mambo mengine, ulilenga kuimarisha maarifa kwa watoa huduma za msaada wa kisheria, kwa kutumia njia mbadala ya utatuzi wa migogoro ya kifamilia, kuongeza uelewa wa jamii kuhusu sheria na kuimarisha mfumo wa kifamilia katika utatuzi wa migogoro kwa kuzingatiwa viwango vya sheria nchini.

Kwa mujibu wa Mandari, faida nyingine ya ADR ilikuwa ni kuokoa gharama, kwa sababu unapofungua shauri mahakamani, kuna gharama za ada unatakiwa kulipia, lakini kupitia mradi huo hakuna gharama hivyo punguza mrundikano wa kesi mahakamani.





# Barabara ya Kahama-Kakola yapata mkandarasi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BARABARA korofi kutoka Kahama mkoani Shinyanga hadi Kakola mkoani Geita yenye urefu wa kilomita 73 imepata mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami hali itakayorahisisha shughuli za usafiri.

Imeelezwa kukamilika kwa barabara hiyo pia kutarahisisha usafirishaji mazao ya biashara pamoja na madini kutoka Mgodi wa Barick Bulyanhulu.

Barabara hiyo iliyojengwa kwa kiwango cha changarawe inatajwa kuiingizia hasara serikali kwa kuhitaji marekebisho ya kila mwaka kutokana na ubovu wake unaosababishwa na shughuli za usafirisha wa mizigo mikubwa yakiwamo makinikia kutoka migodini.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alipongumza na wakazi wa Kijiji cha Bunva Kata ya Segese Msalala katika a ziara yake kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi.

Alisema serikali imepokea kero ya barabara hiyo inayounganisha mikoa ya Mwanza, Geita na Kagera na mkandarasi anayetakiwa kuijenga amesha-patikana huku zaidi ya Sh. bilioni 90 zikitarajia kutumia katika utekelezaji wa mradi huo.

Alisema serikali inatarajia kufunga mkataba na mkandarasi huyo ifikapo Januari Mosi, 2024 na kuwaagiza waliojenga kwenye hifadhi ya barabara kuondoka haraka ili wasije kuwa sehemu ya kukwamisha mradi huo.

Vilevile alisema, serikali imekuwa ikiunganisha mawasiliano ya barabara kila mwaka wa fedha kupitia TANROAD na TARURA wilaya hadi mikoa kwa kurekebisha barabara za lami zenye changamoto na kuzijenga upya barabara za changarawe ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya chakula na biashara kutoka shambani hadi sokoni.

Diwani wa Kata ya Segese, Joseph Manyala, alisema ubovu wa barabara hiyo umesababisha gharama kubwa ya usafirishaji wa mazao kutoka shambani hadi sokoni hivyo ujenzi wake utakapoanza na kukamilika utasaidia wakulima kupata fedha za kuendesha maisha yao.

Alisema, wakulima wengi wamepata hasara ya kuharibikiwa na mazao shambani hususani nyanya na mahindi kwa ubovu wa barabara hiyo, na kuomba utiaji saini mkataba wa ujenzi usichukue muda mrefu kwani vijana wanahitaji kazi zisizohitaji ujuzi ili kujiingizia kipata ndani ya familia zao.

Mkazi wa Kijiji cha Bunva, Elizabeth Mahona alisema, ni miongoni waliopewa barua ya kuondoa nyumba yake ya biashara kwakuwa alikuwa ameijenga ndani ya hifadhi ya barabara huku bikoni ikiwa nyuma ya makazi yake, amefanya hivyo ili asije kuwa kikwazo cha kukwamisha ujenzi wake.



Katibu wa Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Samweli Jacksoni (kushoto), akikabidhi ng'ombe kwa Mkuu wa Magereza Wilaya ya Shinyanga, Theomphil Mulokozi, kwa niaba ya Mbunge Patrobas Katambi na Mbunge wa Viti Maalum, Santiel Kirumba, kwa ajili ya wafungwa na askari Magereza kusherehekea Sikukuu ya Krismasi juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wabunge wawakumbuka wafungwa sikukuu Krismasi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MBUNGE wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu na Mbunge wa Viti Maalum wa mkoa huo, Santiel Kirumba, wametoa ng'ombe kwa wafungwa wa Gereza la Wilaya ya Shinyanga kwa ajili ya kusherehekea sikukuu ya Krismasi.

Ng'ombe huyo alikabidhiwa Juzi na Katibu wa Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Samweli Jackson kwa niaba ya wabunge hao, kwa Mkuu wa Gereza hilo Theophil Mulokozi ikiambatana na Sh.200,000 kwa ajili ya sabuni.

Samweli alisema zawadi hiyo ni sehemu ya kutekeleza ahadi ya wabunge hao kuwawezesha askari Magereza pamoja na wafungwa washerehekee Sikukuu ya Krisimas kwa furaha na upendo.

"Ng'ombe huyu anathamani ya Sh. 700,000 pia nimekabidhi Sh.200,000 ambazo zimetolewa na Mbunge Katambi kwa ajili ya kununua sabuni za kufulia ni moja pia ya ahadi yake kwa wafungwa," alisema Samweli.

Mkuu wa Gereza hilo, Theophil Mulokozi, aliwashukuru wabunge hao kwa kuwakumbuka wafungwa na askari magereza na kutoa wito pia kwa viongozi wengine kuwa na utaratibu wa kuwambuka katika sherehe mbalimbali.

Wakati huo huo , Mkurugenzi wa kampuni ya 'Agab Hardiwere & Timber supply', iliyopo wilayani Chato, Mkoa wa Geita, Aloyce Mwenda, aliwakumbuka wafungwa na mahabusu wa gereza lilipo wilaya hiyo hao kwa kutoa mchele, kondoo, sabuni, mafuta ya kupaka, chumvi, vitafunwa na nyembe kwa ajili ya usafi.

Akipokea misaada hiyo kwa niaba ya wafungwa na mahabusu, Kaimu mkuu wa magereza hiyo Mkaguzi Msaidizi wa Magereza Pius Samba alizipongeza baadhi ya taasisi makampuni na watu binafsi walioguswa kusaidia wahitaji hao kwa kuwa suala hilo ni la kimungu.

**Imeandikwa na Marco Mduhu (SHINYANGA) na Daniel Limbe(CHATO)**

# WAMACU yajitosa vita ya uhaba wa chakula

**Na Timothy Itembe,** MARA

CHAMA Kikuu cha Wakulima cha Mara Cooperative Union (WAMACU) kimejitosa katika mapambano dhidi ya uhaba wa chakula, lishe na umaskini mkoani humo kwa kuweka mpango wa kushirikiana na serikali kuhakikisha wakulima wanalima kwa tija.

Meneja Mkuu wa chama hicho, Samweli Gisiboye, alisema hayo kwenye Mkutano wa Bodi ya WAMACU uliolenga kujadili na kupitisha mpango wa maendeleo ya miaka mitano ijayo.

"Tunahitaji kushirikiana vyema na serikali kukabiliana na baa la njaa ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango huu ambapo malengo, shabaha, shughuli na mikakati imeandaliwa kwa kipindi cha miaka mitano ijayo ukiwa na lengo la kufikia 2023-2028 tuwe tumepunguza kiwango cha njaa na umaskini kwa wananchi," alisema Gisiboye.

Mwenyekiti wa WAMACU, David Hechei, alisema kwa msimu wa 2023/2024 wamekusamya jumla ya kilo 571,747 kutoka vyama vya wilaya ya Tarime DC na TC.

Alisema kati ya hizo kilo 47,098 zilitoka JKT Ng'ereng'ere ambazo zimeingizwa katika wilaya Tarime, DC na jumla ya kilo 1684 zilitoka kwa Masisita Kitenga na kuingizwa katika wilaya ya Rorya.

Mhasibu wa WAMACU, Mohamed Sakilu, alisema katika msimu wa 2023-2024 chama kimetumia zaidi ya Sh. bilioni 3.37 kwa ajili ya kukusanya kahawa na kurejesha mkopo wa msimu uliopo 2022/2023 wa zaidi ya Sh.milioni 514.2 pamoja na shughuli za uendeshaji wa biashara ya kahawa.

Wajumbe waliohudhuria kikao hicho, Momanyi Range ambaye ni mwenyekiti wa Jukwaa la wakulima Mkoa Mara, alisema lengo la kikao ni kuhakikisha mkulima ananufaika na WAMACU kupitia masoko bei nzuri pamoja na kupatiwa miche ya kahawa.

Mwenyekiti huyo alisema WAMACU wamepanua wigo wa kusambaza mbolea ya ruzuku ya serikali kwa bei elekezi na wanahakikisha mkulima anaipata kwa ukaribu na kuacha kwenda kununua nchi jirani Kenya Kwa bei ya magendo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 26, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI




Ukurasa 14

## Msongamano, foleni barabarani ulivyotesa 2023, kuendelea tena



Ukurasa 13

## Kutoka kuazima ardhi hadi kumiliki shamba la miti

NA SABATO KASIKA

# Karibu mwaka 2024, wadau elimu wanatamani kufeli 'English' kukome



KATIKA dunia ya leo, Kiingereza kina nafasi kubwa, kwa kuwa huzungumzwa zaidi duniani na kinaweza kuongeza uwezekano mkubwa wa kupata nafasi nyingi ziwe kiuchumi na kijamii kutokana hadhi yake kimataifa.

Mathalani, ukitaka kujua umuhimu wa lugha hiyo ingia kwenye usaili, lugha inayotumika ni Kiingereza, iwapo hukijui safari ya kutafuta ajira inaweza kuishia hapo, hivyo kujua Kiingereza katika dunia ya leo kunaweza kuwa na umuhimu wa kipekee kwa Mtanzania.

Pamoja na umuhimu huo, Watanzania wanatarajiwa kuwa walimu na wakufunzi wa Kiswahili duniani, ambao lazima wazungumzie somo kwa Kiingereza kisha waanza kulifundisha kwa Kiswahili, mfano 'we are going to learn synonyms' 'leo tunajifunza visawe mfano; ua 'mmea au kutoa uhai...". Ndipo ulipo umuhimu wa kiingereza.

Leo lugha hiyo imekuwa ni mfupa mgumu kwa wanafunzi karibu wa ngazi zote, hata matokeo ya darasa la saba ya mwaka huu, Baraza la Mtihani la Taifa (NECTA) linaeleza kuwa wanafunzi wamefanya vibaya katika mtihani wa Kiingereza, hali inayoonyesha kuwa jitihada zaidi zinahitajika unapozungumziwa mtangamano wa Afrika na Afrika Mashariki mbao una fursa nyingi ambazo huenda zikawapita Watanzania kwa kutokujua Kiingereza.

Tunapoeleka kuagana na mwaka 2023, baadhi ya wadau wa elimu, wanatoa ya moyoni kuhusu ugumu wa lugha hiyo kwa Mtanzania ambaye alitakiwa aifahamu na nini kifanyike isiwe ngumu kuzifikia na kuzitumia fursa lukuki zilizo mbele yake.

**LILIPO KOSA**

Mbunge mstaafu wa CHADEMA aliyewahi kuwa Waziri Kivuli wa Elimu, Suzan Lyimo, anasema, katika karne hii Kiingereza hakikwepeki na kwamba kinachosababisha wanafunzi wasikimudu, ni kukosekana walimu mahiri wanaokijua vizuri.

Suzan anashauri 2024 uwe wa serikali kuwekeza kwa walimu ili waondokane na changamoto zinazochangia washindwe kufundisha kikamilifu na kusababisha wanafunzi wafanye vibaya.

'Nilishasema kuhusu uwekezaji katika elimu kwamba sio kujenga majengo mazuri, ni walimu hasa, serikali ihakikishe inakuwa na walimu bora wanaoweza kuleta ushindani," anasema Suzan.

Anafafanua kuwa kinachotakiwa ni kuwapa walimu maslahi mazuri, marupurupu, mahali pazuri pa kuishi na kupunguza idadi ya wanafunzi katika chumba cha darasa.

Anasema:"Kutothaminiwa kwa walimu kunasababisha baadhi yao kwenda shuleni na biashara ndogo na kuanza kuuza hata wakati wa vipindi ili kujikimu kimaisha."

"Lakini pia shule za serikali hazina walimu mahiri wa lugha hiyo. Mwalimu hajasomea Kiingereza anaambiwa akafundishe ni kwamba wanafunzi wanafundishwa lugha hiyo na mwalimu asiyeijua, matokeo yake ni kupata sifuri."

Mwalimu huyo mstaafu wa Jangwani, anasema, anatamani kuona walimu wanapata mafunzo mazuri ya lugha, ili kusaidia wanafunzi kudumu lugha hiyo ili nao waendane na wakati hasa kipindi cha utandawazi.

"Kawaida, mwalimu anatakiwa afundishe masomo mawili, lakini anafika shuleni anaambiwa afundishe yote hata yale asiyoyajua, matokeo yake ni kuendelea kuua elimu. Mwaka 2024 uwe wa mabadiliko," anasema.

**SIASA KANDO**

Meshack Kapange ni Katibu wa Chama cha Kutetea Maslahi ya Walimu Tanzania (CHAKAMWATA), anayesema, ili wanafunzi wamudu lugha hiyo, siasa ziachwe pembeni.

Kapange anasema mtindo wa kuteua watu kwenye nafasi ambazo si taaluma zao, ndiko kunakosababisha hayo yote, kwa kuwa hawawezi kuwa na ubunifu wowote kwa kitu ambacho hawajakisomea.

"Ninatolea mfano miaka ya nyuma wamewahi kuteuliwa mawaziri wa elimu wakaunganisha baadhi ya masomo, kuondoa masomo ya biashara, mara ukaja mfumo wa walimu wa 'voda fasta' wa kidato cha sita kwenda chuo miezi michache na kuja kufundisha," anakumbusha Kapange.

Imekuwa ni jambo la kawaida mwenye taaluma ya udaktari wa watu au aina nyingine ya taaluma kuteuliwa kuwa waziri wa elimu na kushindwa kufanya kazi ipasavyo kwa kuwa si eneo lake.

"Sisi wakati tupo chuo cha ualimu tulikuwa tukiandaliwa kuwa walimu wa masomo yote ya shule ya msingi, kwani tunakua na uwezo wa kufundisha somo lolote, lakini utaratibu huo haupo tena," anaeleza.

Anasema, kwa sasa mwalimu wa shule ya msingi anachagua masomo mawili ya kufundisha kama wa sekondari au chuo, na kwamba wengi wanakimbilia masomo mapesi kama stadi za kazi na haiba na michezo.

INAENDELEA UK. 12

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Waraka kwa wazazi na walezi, unapoelekea kumaliza mwaka



MZAZI au mlezi unapokaribisha mwaka mpya ambao muhula wa kwanza unaanza Januari 8, unamtazamaje mtoto wako tofauti na ilivyokuwa 2023?

Binti au kijana anaingia darasa la kwanza, la nne au saba ama yuko chuo kikuu na unataka afaulu, uanze kumfuatilia, kujue anachofanya shuleni usiishi kimazoea, kama ilikuwa kawaida yako ongeza bidii.

La msingi ni kujua kwamba mtoto vile umleavyo ndivyo akuavyo na samaki akunjwe angali mbichi, inamaanisha kwamba jinsi utakavyomlea mtoto wako tangu udogoni ukamfunza maadili na kumuelewesha umuhimu wa tabia njema, kusoma au elimu na kumpenda Mungu ni mwanzo wa kufaulu.

Na kama utakwenda kinyume na hayo Katika malezi hayo akakua akapenda kwenda shule na kusoma kwa bidii ndivyo atakavyokuwa katika maisha ya kuelekea kutimiza ndoto zake kielimu.

Wazazi na walezi ikiwa shule inaanza tena Januari 8, 2024 iwapo mwanao anaanza darasa la kwanza au anaendelea na masomo mzoeshe kulala na kuamka mapema ili asiwe anachelewa kwenda shuleni wala asisumbue anapotakiwa kujiandaa asubuhi.

Haya ni ya muhimu kwa watoto wa shule za msingi, kumbuka akizoea hatapata taabu ya kuamshwa amshwa kwa sababu siku za usoni atakuwa anaamka mwenyewe na kujitegemea. Hakikisheni pia usafi wa watoto kabla hawajatoka.

Wakagueni kama wameoga na wamevaa sare za shule ambazo ni safi. Kumbukeni suala la soksi ambalo mara nyingi mwanafunzi anazivaa wiki nzima bila ya kuzifua, linaweza kuwa kero.

Usiache kumnunulia pea nyingi za soksi na ukague iwapo zinafuliwa na umkumbushe kuzivua kama ni mdogo mfulie kila wakati. Kumbuka soksi chafu zinasababisha maradhi ya miguu na kuleta harufu mbaya anapovua viatu au popote anapokuwepo miguu inanuka na kukera wengine.

Suala la daftari, vitabu na begi ni muhimu kwa hiyo wazazi, hakikisheni mtoto anabeba begi la shule safi lenye mkebe wenye kalamu, penseli, kifutio, kichongeo, rula, madaftari yote na vitabu.

Ni vizuri mzazi ukajua ratiba ya masomo ili abebe yale madaftari ya siku ile badala ya kujitwisha begi lililojaza kila kitu ambacho hakina sababu kwa siku hiyo.

Watayarishieni watoto kitu chochote cha kula kabla hajaondoka na hasa kama ni mwanafunzi wa kutwa. Ni vizuri wakapata chai ya moto na vitafunwa, ni vyema kumpa chakula cha mchana kwasababu mara nyingi ratiba ya shule inakwenda mpaka jioni. Hivyo ni busara kama kuna utaratibu ambao umewekwa na shule wa wazazi kulipia ili wanafunzi wapate chakula cha mchana, kuwapa hela si jambo jema kunawachanganya wanafunzi kupenda na kuzoea fedha.

Chukua namba za walimu ili kuwasiliana nao kuhusu maendeleo ya mwanafunzi shuleni kimasomo, nidhamu na afya kumbuka kuna wakati wazazi na walezi wanapigiwa simu na matapeli kuwa mtoto amelazwa au amezimia na kutakiwa kutuma pesa utayaepuka kama una namba za walimu wake ili wakuthibitishie.

Tafuta namba za mkuu wa shule, mwalimu wa darasa, taaluma, nidhamu na kama ni mwanafunzi wa bweni pata pia namba ya mlezi wa kiume au wa kike. Na mlezi wa karibu na ndiyo wa kuanza naye akiwa shuleni ni mwalimu wa darasa.

Wazazi na walezi hakikisheni mtoto akirudi nyumbani, unakagua madaftari yake ili kujua kaandika nini kwasababu unaweza ukadhani kwamba katoka shuleni kumbe hajafika na siku moja unaweza kuletewa kesi kwamba mwanao ni mtoro na notsi darasani haandiki na ukaanza kushangaa imekuwaje kumbe kosa ni lako, hukumfuatilia mtoto toka mwanzo.

Mwandalieni mtoto ratiba ya kujisomea akiwa nyumbani. Kwa wanafunzi wa bweni wao wanayo ratiba maalum inayosimamiwa na shule na kwa huyu wa kutwa, msimamizi ni wewe mzazi au mlezi na huo ni wajibu wako na bila hivyo lengo halitafikiwa.

**KUTIMIZA NDOTO**

Ni jambo la msingi sana kumweleweshа mtoto umuhimu wa kuwa na ndoto katika maisha yake na hapa ambayo ni yeye anafikiria awe nani katika maisha yake ya baadaye. Anasoma ili awe nani? Mataifa yaliyoendelea Ulaya na Marekani wanafanya mapema kwa watoto wao wangali wadogo na Watanzania pia wajifunze yale mazuri kama hayo.

Kwa mfano, iwapo ni kuwa daktari, mchora majengo, mhandisi, rupani au mfanyabiashara mkubwa ni masomo yapi ya kuzingatia? Kwa shule ya msingi mhimize kupenda hisabati na sayansi , lakini kwa sekondari asisahau hisabati.

Yote yatategemea anachokitamani ambacho mzazi ataangalia kwenye tahsusi anayoipendelea mfano Physics, Chemistry na Biology (PCB). Mhasibu au mchumi ni Economics, Commerce na Accountancy (ECA), lakini hisabati ni lazima awe vizuri.

Ikumbukwe ndoto ya mtoto itaanza kutimia pale atakapofaulu mtihani wake wa taifa wa kidato cha pili na ikawa yale masomo ya ndoto yake ameyafaulu. Hii maana yake ni kwamba Mwalimu wa Taaluma kwa kawaida huwapanga wanafunzi kwenye michepuo yao kutokana na ufaulu wao wa Baraza la Mitihani.

Kwa mfano mtoto anapenda kuwa daktari lakini masomo ya sayansi yote anapata F haiwezekani asome sayansi kuanzia kidato cha tatu kwasababu inaonesha kuna udhaifu katika masomo hayo. Kwahiyo, mwalimu atampeleka kwenye mchepuo unaoendana na ufaulu wake.

**KUMBUKA ZAWADI**

Mtoto ajiandae na mitihani vizuri na si mitihani ya taifa bali hata ile ya ndani wanayopewa na shule au inayotoka shule mbalimbali kwa ajili ya kuwapima wanafunzi. Ni vizuri kila mtihani anaofanya mwanao akuonyeshe na kama amefeli muulize imekuwaje. Na kama kashika nafasi ambayo hairidhishi aulizwe, kwanini asiwe katika 10 bora"?

Wazazi na walezi wawape moyo watoto kadri wanavyofanya vizuri na kama kuna uwezekano wa zawadi kama motisha, mnunulie na akifanya vibaya usimkatishe tamaa, mtie moyo zaidi na zaidi.

Kitu cha muhimu kwako ni kufuatilia maendeleo ya mtoto wako akiwa shuleni na kuwasiliana na walimu ili kujua uhalisia wa hali yake kimasomo, nidhamu na matarajio na daima uwakumbushe upendo kwa mama, baba, ndugu zake na kila mmoja na pia kumpenda na kumwogopa Mungu.

# Karibu mwaka 2024, wadau elimu wanatamani kufeli 'English' kukome

**INATOKA UK. 11**

"Mtindo huo unaosababishwa na siasa, inachangia somo la Kiingereza kukosa walimu na kuwafanya wanafunzi wasilijue. Hivyo kama tunataka twenda vizuri mwaka ujao, siasa zikae pembeni," anasema.

**TUJIPANGE UPYA**

Katibu wa Chama cha Wamiliki wa Vyuo na Shule binafsi Tanzania (TAMONGSCO), Benjamin Nkonya, anasema tatizo la kutoelewa lugha linajitokeza kila mwaka, na kwamba kuna haja ya kubadili uelekeo.

"Kiingereza na hisabati ni masomo ambayo wanafunzi wanafanya vibaya kila mwaka, tangu ukoloni hadi leo hatujawa vizuri, ni vyema turudishiwe Kiswahili hadi tutakapomudu lugha," anashauri Nkonya.

Anafafanua kuwa wanafunzi wamefanya vizuri Kiswahii, na kwamba ana uhakika wakifundishwa kwa lugha yao wanaweza kuelewa vizuri kuliko ile ambayo hawaijui. "Sio kwamba Kiingereza kiachwe, bali tutafute njia sahihi ambayo itawawezesha kukimudu, kwani inaelezwa kuwa kidato cha kwanza cha pili, wanafunzi wamekuwa wakipata shida kutokana na kukosa msingi bora wa lugha hiyo," anasema.

Kwa kuwa kila mwaka matokeo ya Kiingereza huwa ni mabaya, anaona kuna haja ya kujipanga upya mwaka ujao kwa kuweka mikakati ambayo itasaidia wanafunzi kuimudu.

"Hatuwezi kujitenga na dunia, hasa kwa kutambua kuwa Kiingereza ni lugha kubwa ya kimataifa ambayo ni muhimu wanafunzi wetu waimudu ili waweze kuingia kwenye soko na mipango ya maendeleo duniani," anasema.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU, NJOMBE

## TASAF MKOMBOZI KAYA MASKINI

# Kutoka kuazima ardhi hadi kumiliki shamba la miti

Ni kikundi cha watu 11 ambacho kinachoundwa kutoka kwenye kaya maskini zinazonufaika na Mradi wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF).

Kikiwa na wanachama watatu wanaume na wanawake wanane, wanaanza kilimo cha miti kwa kuazima shamba na hatimaye kufanikiwa kumiliki lao wenyewe lenye ekari mbili wakilinunua kwa Shilingi milioni 1.1.

Mwenyekiti wa kikundi hicho kinachojulikana kama Asante, Joyce Kilasi, anasema walianza mwaka 2016 wakati walipochukua awamu ya kwanza ya fedha za TASAF na kushauriana na wanachama wenzake kuazima shamba ambalo walipanda miti na ilipokomaa waliiuza na kununua shamba lao wenyewe.

Kupitia faida waliyopata baada ya kuuza mazao yao ya miti, wamefanikisha kila mwanachama kujenga nyumba ya matofali ya kuchoma iliyoezekwa kwa bati.

"Kwenye kikundi chetu kila mwanachama amejikomboa kutoka kwenye nyumba za kupanga au kuishi kwenye mabanda ya nyasi na sasa kila mmoja wetu amejenga nyumba yake mwenyewe na imeezekwa kwa bati," anasema Mwenyekiti Joyce kwa kujivunia mafanikio hayo.

Vile vile, anasema kama mmoja wa wanachama amekwama kukamilisha nyumba yake, wanachama wenzake humsaidia ili aweze kuikamilisha.

Kupitia fedha za TASAF na faida wanayopata kutoka kwenye shamba lao la miti, hivi sasa kila mwanachama anashughuli yake binafsi inayomwezesha kujiimarisha kiuchumi kupitia biashara anayofanya.

"Kati yetu kuna wenye maduka, wapo wanauza mitumba, wafugaji na wanaofanya kilimo, hizi shughuli tunazifanya nje ya mradi wetu wa shamba," anasema Joyce.

Kuhusu mradi wa chamba la miti, anasema huanza kuvuna baada ya miaka sita kama watauza miti hiyo kama vigogo ambavyo hutumika kusagwa na kutengeneza bidhaa mbalimbali za samani na wateja wakubwa wanaonunua bidhaa hiyo na kampuni za Wachina.

Vilevile, wakiamua kuuza kama miti ya nguzo husubiri mpaka baada ya miaka minane ndipo inapokuwa imekomaa vizuri na mti mmoja wa nguzo huuzwa kwa Sh. 30,000.

Kupitia fedha wanazopata kwenye mradi wao wa shamba la miti, wanufaika hao wamefanikiwa kuanzisha kikundi cha kuweka na kukopa (VIKOBA), ambacho huchangia kuanzia Sh. 5,000 hadi 10,000 na huruhusiwa kukopa kila Alhamisi.



Mwenyekiti Joyce Kilasi, akionyesha shamba linalomilikiwa na kikundi anachokiongoza. PICHA: MWANDISHI WETU

Fedha za TASAF hutolewa kwa idadi ya ukubwa wa kaya kwa mfano kuna wanaopokea Sh. 36,000 kwa mwezi na kuziingiza kwenye miradi wanayoamua kuianzisha ikiwamo ufugaji, kilimo, biashara kwa mujibu wa kaya inavyoamua.

Wanakaya waliokuwa katika hali ya umaskini wa kutisha sasa hivi ambao kabla ya kuingizwa kwenye mpango walikuwa wanashindia mlo mmoja, sasa wanaweza kumudu milo mitatu kwa siku na kupitia miradi yanayoifanya, fedha hizo zinawasaidia kupeleka watoto shule na kununuliwa mahitaji muhimu kama sare na madaftari.

Benita Stephan, mnufaika wa TASAF ambaye ni mmoja wa kikundi cha Asante, anasema alianza kunufaika na fedha za mpango kwa kupokea Sh. 36,000 na alipopata alinunua nguruwe wawili wa kike na wa kiume ambao walizaa na kuuza baadhi na fedha walizopata kutoka kwenye mifugo hiyo waliza kujenga nyumba.

"Nashukuru sana TASAF imeniokoa, nilikuwa maskini sana chakula cha shida, lakini sasa nina shamba na nimeweza kuongeza ng'ombe ambaye ninamfuga ananipatia maziwa ninauza," anasema.

Mnufaika Rehema Kilasi, mmoja wa wanachama wa kikundi cha Asante, anasema kupitia faida anayopata kwenye VIKOBA kila mwaka wanapovunja, imemsaidia kufanya shughuli mchanganyiko ambayo humpatia maokoto yake na kuweza kumudu maisha.

"Mimi nafanya shughuli mbalimbali, nalima nyanya, viazi, nafuga na vile vile nina kiduka changu, hivyo maokoto yangu yanapata kwenye mashamba yangu na biashara yangu ya duka," anasema.

Anasema matarajio yake kupitia maokoto anayopata kwenye shughuli zake ni kufungua duka kubwa la jumla katika kijiji chake.

Ushauri wake kwa wanufaika wa mpango huo ni kuwa fedha za TASAF sio za kula bali ni za kuanzishia miradi ambayo itamwezesha mtu kufanya shughuli endelevu ya kumwingizia kipato.

Bwana Shamba wa Kata ya Kichiwa, Salivius Kawogo, anasema jukumu kubwa analolifanya kuwasaidia wakulima walengwa wa TASAF ni kufuata kanuni za upandaji miti ili mashamba yaweze kukua vizuri na kupata mavuno bora.

"Pia tunawaelimisha kila mlengwa anayefanya kilimo awe na miti 10 ya miparachichi, lengo ni kuwasaidia mradi utakapoisha waweze kusimama wenyewe," anasema Kawogo.

Kelvin Kapungu ni Mratibu wa TASAF, Njombe ambaye anasema Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ina wanufaika zaidi ya 3,000 na walengwa 137 wanajishughulisha na shughuli mbalimbali ikiwamo vikundi vya kuweka na kukopa.

Kapungu anasema matokeo ya kikundi cha Asante, malengo yao yanaendana na kuwa na miradi endelevu, kilianza kwa kuazima shamba na sasa wana ekari mbili na kila mwanachama anashughuli binafsi ya kufanya.

Anasema wanufaika wanapokuwa na vikundi vyao vinawawezesha kuwapa faraja ya kufanya jambo lao.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kuendeleza mpango huu na kuona thamani yake kwasababu fedha zinasaidia katika mpango wa mradi wa parachichi, walengwa wameamua kukatwa fedha zao kwenye dirisha kwa ajili ya kununua miche ya zao hilo," anasema Kapungu.

**KILIMO CHA PARACHICHI KAYA ZA WANUFAIKA**

Katika jitihada za kuendelea kuzijengea kaya za wanufaika wa TASAF ili kuweza kujitegemea, Mkoa wa Njombe umeanzisha mradi maalum wa kilimo cha parachichi ambacho kila kaya yenye eneo na itakayoridhia itawezeshwa angalau miche 10 ya kuanzia.

Matarajio ya mkoa huo ni baada ya miaka mitano ijayo kila kaya inatarajiwa kuwa na uwezo wa kuzalisha matunda yatakayoziingizia kipato kisichopungua Shilingi milioni mbili.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka amezindua mradi huo Januari, mwaka huu na utekelezaji unafanyika kwa awamu kwa kaya zote 24,876 za wanufuaika ndani ya mkoa huo.

Awamu ya kwanza ya utekelezaji umeanza, kaya zote 1,804 zilizokidhi vigezo (utayari wa kuwa na eneo la kudumu) katika Halmashauri ya Mji wa Makambako zimewezeshwa kati ya mche mmoja hadi 20 na zinaendelea kuitunza kwenye mashamba yao chini ya wataalamu wa kilimo tangu Machi, mwaka huu.

Maandalizi ya utekelezaji wa mradi huo katika halmashauri zilizosalia yanaendelea na unatarajiwa kufanyika mwenzi kuanzia Machi nwakani.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Msongamano, foleni barabarani ulivyotesa 2023, kuendelea tena




Foleni kwenye moja ya barabara mkoani Dar es Salaam ni tatizo 'endelevu'. PICHA: MTANDAO

WATANZANIA wanapoingia 2024 Nipashe 'Team', tunawatakia heri na mafanikio kwa mwaka mpya. Licha ya kufurahia kuvuka, tunaangalia mambo ambayo wanaingia nayo wakati wanasherehekea ujio wa mwaka mpya.

Tukichambua baadhi ya kero msongamano na foleni maeneo mbalimbali ya kupata huduma umeendelea kuwa chanzo cha kupoteza muda mwingi kusubiria raia wapate kile wanachotaka kwa mwaka unaomalizika Jumapili Desemba 31.

Wasomaji wetu wakumbuke kuwa shida hii haijaanza leo ni sugu tena wataendelea nayo hivyo wazidi kujipanga kisaikolojia kuikabili na kiasi ufumbuzi unavyokosekana pengine changamoto hiyo ya msongamano na foleni itakuwa kubwa zaidi kwa vile watu wanazidi kuongezeka, wakielekea kufikia milioni 62 sasa.

Wengi ni mashuhuda kuwa ni vigumu kukwepa foleni na misongamano kwenye vivuko iwe baharini, ziwani au kwenye mto. Ni tatizo kwenye kusaka maji ya kunywa hasa wakati wa kiangazi, kadhalika ndani ya daladala na mabasi ya mwendokasi pamoja na hospitalini huko nako usiseme.

Watanzania wengi licha ya kuendelea kuwa waathirika wa tatizo hilo hawajashtuka kuwa muda ambao ungetumika kwa ajili ya kuzalisha na kubadilisha maisha unapotea kila siku hasa kwenye foleni na kusubiri huduma.

Mathalani, shida ya foleni hospitalini hasa kuwaona mabingwa hata kupimwa maabara inaendelea kutesa kila wakati kwa kulazimisha wagonjwa au jamaa zao kujihimu saa 10 alfajiri kuwahi namba za matibabu.

Hata hivyo kuamka pekee si ufumbuzi kwa kuwa wataendelea kusubiri kumwona mbobezi, kufanyiwa vipimo na kurudi tena kwa daktari baada ya uchunguzi, yote hayo yakitumia siku nzima licha ya kuamka saa 10 alfajiri.

Ni wazi kuwa kama ni mmoja wa wanafamilia amempeleka mtoto au jamaa hospitalini hatafanyakazi kutwa badala yake atamaliza siku bila kufanya jukumu la kujipatia kipato. Licha ya kuumiza mtu binafsi ni wazi kuwa hata uchumi wa taifa nao unaathirika.

Kusongamana kwenye vyombo vya usafiri kwenye foleni ndani ya majiji na miji mikubwa nalo ni tatizo wanalovuka nalo mwaka 2024 abiria wanachoka kupindukia, kuchafuka kwa kukanyagana, wenye afya kwa upande mwingine huambukizwa maradhi, wengi wananung'unika yote hayo yakiathiri afya ya akili.

Katika hili baadhi ya wasafiri wanaotumia mabasi ya mwendo kasi jijini Dar es Salaam hulalamikia magari kuchelewa na msongamano mkubwa.

Shida ya usafiri huo wa daladala na vivuko huchangia kuleta utovu wa nidhamu, vurugu, wizi na hata kuumizana, mfano kugombania magari. Watu wanakanyagana, kuingilia madirishani, kuibiana, abiria kuzidi uwezo wa chombo, kuumiza watoto, kurushiana maneno makali na wakati mwingine wagonjwa kuumizwa.

Yote hayo yanafanyika ili kuwahi nafasi kwenye chombo cha usafiri, athari za vurugu hizo ni pamoja na kuharibu vyombo vya usafiri mathalani kuvunja vioo, milango, vitasa lakini pia kwa wanaoumia kutofanyakazi au wanaopoteza mali kama simu, pesa na bidhaa walizonunua kupata hasara na kurudi nyuma kiuchumi kwao binafsi, familia na Tanzania.

Wakati mwingine foleni kwenye ofisi za umma mfano wilayani, idara ya ardhi, kuomba vibali, mahakama, wizarani, polisi, shule na vyuoni huwalazimisha wanaohitaji huduma kutoa mlungula kwa maana ya toa kitu upate kitu.

Kutoa rushwa ni kuondoa haki. Kama vile ahadi za Mwana TANU zinavyosema kuwa rushwa ni adui wa haki. Usipokee wala kutoa rushwa, tena ni sumu kwenye jamii kwa vile si maadili.

Kukosa maadili kunaibuka pale wale wanaojua kuwa ili kutoa huduma ni lazima wahongwe fedha, hujenga mazingira ili kupata rushwa wakati wote na kuongeza hasara kwa wananchi maskini ambao wanalazimika kusaka mlungula.

Kwa mfano kupata huduma mahakamani, kusaka uhamisho wa mwanafunzi kutoka shule ya msingi au sekondari ili kuhamia kwingine, kuomba mkopo kwenye taasisi za kifedha au hata kazi za zabuni za ukandarasi kwenye ngazi mbalimbali.

Foleni na msongamano unaendelea kuwa mwanzo wa utajiri kwa wengine japo wapo watakaopata umaskini. Mfano baadhi ya watu ambao huficha bidhaa, kuchakachua na kutoa bidhaa mbovu kwa wananchi wakitumia mwanya kuwapo tatizo la foleni na msongamano. Mfano mwaka unapomalizika tatizo la mbolea ya ruzuku kuwafikia wakulima lilikuwa kubwa na wakulima wakalalamikia kitendo hicho wakidai kuwa baadhi ya mawakala wanaficha mbolea ya ruzuku .

Januari 2023 mbolea ya ruzuku kwenye mikoa ya Songwe na Mbeya iliuzwa hadi Shilingi 90,000 kwa mfuko wa 'yurea' badala ya 70,000 bei elekezi ya serikali kutokana na masuala yanayohusiana na msongamano na foleni wakulima wakifuatilia pembejeo hizo. Hali iliyoleta utajiri kwa wauza mbejeo na umaskini kwa wakulima.

**2024 NI UFUMBUZI**

Watu hawawezi kukaa kimya maji yakiwafika shingoni ikiwezekana serikali ishirikishe umma kupata majibu ya kero ambazo kila mwaka zinaendelea kuishi na kukua mfano foleni za daladala, vivuko na mwendokasi.

Pamoja na msongamano wa abiria unaotisha kwenye vyombo hivyo hasa asubuhi na jioni, kwa pamoja wafanye tafiti na kupata majibu ya namna bora ya kukabiliana nazo.

Pia kujifunza kutoka kwa mataifa mengine jinsi ya kukabiliana na foleni na msongamano kwenye huduma kuanzia hospitali za mikoa, kanda na taifa na pote kwenye huduma za umma.

Utafiti utatoa majibu ya matatizo hayo kwa kuleta ufumbuzi wa muda mrefu, mfupi kwenye maeneo yote ambayo kila mwaka yanazidi kuwa matatizo ambayo yanakua na kuongeza kero.

Ikumbukwe kuwa shida ya mwaka huu inazidi kuongezeka ifikapo 2024 kutokana na idadi ya watu kuongezeka kila wakati na kuwa uwepo wa watu wapya zaidi wanaotafuta huduma iwe ya usafiri, tiba, polisi na elimu.

Msongamano na foleni barabarani unaweza pia kumalizika kwa kuanza ushirikiano kwenye usafiri. Magari ya serikali na ya binafsi kusaidia kubeba abiria hasa wanafunzi.

Hata hivyo, kuangalia vipaumbele nalo ni jambo muhimu mfano ujenzi zaidi wa miundombinu hasa reli, kufikisha huduma za teknolojia ya mawasiliano ili kufanikisha kuwapa huduma watu hasa maeneo ya vijijini mfano uhamisho wa wanafunzi, kufuatilia masuala ya pensheni, ardhi na usajili wa vitu mbalimbali.

Matumizi ya TEHAMA yanaweza kupunguza msongamano na foleni japo huko nako kuna madai kuwa mafundi wa mitandao wanazijua mbinu za kuchakachua na kuweka mazingira ya kuwanufaisha, hata hivyo juhudi zinahitajika kumaliza tatizo.



# TUGHE yasisitizwa uzalendo utatuzi migogoro kazini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIBU Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, amevitaka vyama vya wafanyakazi (TUGHE) mkoani hapa kuonyesha uzalendo kwa nchi yao kwa kutowatetea watumishi wanaofanya makosa ya kimaadili kazini.

Alisema baadhi ya vyama hivyo vinatetea wafanyakazi waliokosa kwa lengo la kushindana na mwajiri jambo ambalo halileti afya na uwajibikaji kwa watumishi wa umma.

Akifunga semina ya viongozi wa matawi wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) juzi, Dk. Fatuma alivisihi vyama hivyo kutenda haki na sio kumtetea mfanyakazi hata pale anapokuwa amefanya kosa linaloonekana wazi.

"Viongozi wa vyama vya wafanyakazi tubadilike wakati wa kuwatetea wafanyakazi, wakati mwingine tunapitiliza hata pale tunapoona mfanyakazi amekosea tunakwenda kuweka wakili ili mfanyakazi amshinde mwajiri," alisema.

Dk. Mganga alisema wafanyakazi ni lazima watambue kuwa mwajiri anapokuja juu pale mtumishi anaposhindwa kutekeleza majukumu yake ni kwa manufaa ya nchi hasa ikizingatia kuwa wafanyakazi wana mchango mkubwa katika maendeleo.

Aliwaelekeza viongozi wa TUGHE wawasisitize wafanyakazi kuhusu uwajibikaji kazini ili vyama vikawe na tija na faida kwa nchi hasa ikizingatia wanahusika na suala la afya ambalo ni muhimu sana.

"Serikali imetuajiri inatulipa mishahara na inategemea kupata uzalishaji mzuri, wafanyakazi tukiwajibika vizuri tunakwenda kuboresha maisha ya Watanzania wenzetu, hivyo kama wewe ni nesi (muuguzi) au daktari nenda kawajibike katika utoaji huduma kwa dhati ya moyo wote, kwa nguvu zako zote na kwa akili yako yote," alisema.

Alisema wafanyakazi watambue kuwa wamepata ajira kwa neema tu kwani wapo watu kibao wapo mitaani wana elimu hadi ya 'master' lakini hawajaweza kupata ajira.

"Serikali na waajiri hawajakataa kukosolewa, njooni kwa mwajiri kwa staha, ukimkosoa mwajiri bila staha sio afya na hiyo haijengi mahusiano mazuri kazini," alisema.

Aidha, Dk. Mganga aliwataka wafanyakazi kujiepusha na vitendo vya rushwa kazini ambavyo vinaweza kusababisha wafukuzwe kazi kwani serikali haiwezi kumvumilia mfanyakazi anayeendekeza rushwa.

"Tunzeni siri za watu mnaowahudumia, mfano katika sekta ya afya tumesema watu waende na mwenza wake kwa ajili ya kupata huduma sasa mtu amekwenda na mume wa mtu wewe unaanza kusemasema eti sasa huyu si mume wa mama fulani, wewe inakuhusu nini, huo ni utovu wa nidhamu," alisema.

Naye Naibu Katibu Mkuu TUGHE, Rugemalira Rutatina, alisema chama hicho kinatoa mafunzo kwa viongozi ili kuongeza uwajibikaji kwa watumishi na hivyo kutoa huduma nzuri kwa wananchi.

"Tunahimiza suala la uwajibikaji kwa wafanyakazi ili tija ipatikane mahali pa kazi na hivyo kuwa na nguvu ya kudai maslahi yetu," alisema.

Mwenyekiti wa TUGHE Mkoa wa Singida, Dk. Athuman Bunto, aliwataka viongozi kuwa karibu na wanachama ili wanapopata changamoto yoyote kazini wapate ufumbuzi haraka na kuleta morali ya utendaji kazi kwa mtumishi.

Dk. Bunto aliwataka viongozi kuzingatia katiba katika utendaji kazi wao kwani ndio kitawafanya wawe viongozi wazuri wakati wa kutekeleza majukumu yao.




Naibu Katibu Mkuu wa TUGHE, Rugemalira Rutatina, akizungumza na wanachama na viongozi wa matawi katika semina iliyofanyika mkoani Singida mwishoni mwa wiki. **PICHA: TOBIAS MWANAKATWE**

# Bilioni 593.69/- zaboresha huduma ya usafiri Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKOA wa Dodoma umepata jumla ya Sh. bilioni 593.69 kutekeleza miradi ya barabara kwa kipindi cha miaka mitatu ili kuboresha miundombinu na kuondoa changamoto ya usafiri.

Kupitia fedha hizo Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) ulipewa Sh.230.29 na wametengeneza barabara zenye urefu wa kilomita 9248.12.

Vilevile Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) wamewezeshwa Sh. 363.4 kutengeneza barabara zenye urefu wa kilomita 7540.9.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema hayo juzi jijini humo, kwenye kikao cha kwanza cha Bodi ya Barabara kwa mwaka 2023/24 chenye lengo la kuwasilisha, kujadili na kushauri juu ya utekelezaji wa miradi ya barabara za mkoa kwa kipindi cha Julai hadi Novemba 2023.

"Utekelezaji huu wa miradi ya barabara pamoja na miradi mingine ya kimkakati inayotekelezwa hapa Dodoma tuifanye ifanane na matokeo yanayotarajiwa, uwepo wa barabara hizi uendane na kukua kwa uchumi wa wananchi kwani serikali imewekeza ili kuwainua wananchi wake," alisema Senyamule.

Akifungua kikao hicho, Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Ally Gugu, alibainisha majukumu ya Bodi ya Barabara ya Mkoa.

"Bodi ya barabara ya mkoa ina kazi ya kushauri na kutoa maelekezo juu ya maendeleo ya barabara, kutekeleza miradi ya Barabara inayoletwa na serikali, kupokea ushauri kuhusu miradi ya barabara za mkoa na halmashauri pamoja na kutekeleza maelekezo yanayotolewa na Waziri mwenye dhamana," alisema Gugu.

Pia kikao hicho kilifikia maazimio kadhaa ikiwamo TANROADS, TARURA kwa kushirikiana na halmashauri waendelee kuchukua tahadhari kuhusu mvua inayoendelea kunyesha ili kuepuka madhara katika barabara.

"TANROADS na TARURA ziwasilishe jumla ya fidia zinazodaiwa na wananchi wanaopitiwa na miradi ya barabara na ujenzi wa barabara ya makutano ya Kongwa- Mpwapwa ukamilike huku ahadi ya kuanzia Mpwapwa itekelezwe," alisema.

Mkoa wa Dodoma una mtandao wa barabara wenye urefu wa jumla wa kilomita 9248.12 ambao upo chini ya Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) pamoja na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

Kwa kipindi chote cha miaka mitatu wamekua wakitekeleza miradi ya kimkakati ikiwamo ujenzi wa barabara za mzunguko wa nje pamoja na Mradi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa

# Wanaokunywa pombe asubuhi wasakwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa kitengo cha usafi wa mazingira Jiji la Dodoma Dickson Kimaro, amewaagiza watendaji wa kata kuwasaka wananchi ambao wamekuwa wakinywa pombe asubuhi muda ambao wanatakiwa kufanya kazi.

Akizungumza na wakazi wa kata za Miyuji na Mnadani jijini Dodoma juzi, Kimaro aliwaagiza viongozi hao kushirikiana kwenye msako huo ili kudhibiti vitendo hivyo na kuongeza nguvu kazi.

"Kwenye kata na mitaa yenu nyinyi viongozi kuna watu wanakunywa pombe muda wa asubuhi kwa kweli hali hii bado suala la umaskini na uvivu litawaandama familia zinazofanya hivyo, niwaagize wakamateni wote wanaokunywa muda wa saa za kazi," alisema.

Aidha, aliagiza kila mwananchi kuhakikisha kuwa katika eneo lake anafanya usafi wa mazingra badala ya kusubiri kusukumana na vyombo vya kisheria.

"Agizo hili ni utekelezaji wa maelekezo liliyotolewa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, kuhusu wananchi kufanya usafi wa mazingira katika maeneo yenu," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, John Kayombo, aliwataka watendaji hao kusimamia kikamilifu usafi wa mazingira kwa kila mtendaji kwenye eneo lake ili kutimiza wajibu.

"Ninawaagiza watendaji wote wa kata na mitaa kutoa taarifa ya usafi wa kila Ijumaa na ionyeshe eneo lililofanyika usafi, wananchi walioshiriki na hatua zilizochukuliwa kwa waliobainika kuwa na mazingira machafu," alisema.

Kadhalika, aliwataka kutekeleza maagizo hayo kwa kuhamasisha wafanyabiashara na wananchi washirikiane kufanya usafi wa mazingira kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo katika mitaro inayotumika kupitisha maji ya mvua.

"Bado mnatakiwa watendaji wa kata na mitaa kushirikiana na wananchi wenu kufanya usafi wa mazingira kila wakati kama vile kwenye mitaro ya maji ya mvua, ikiwemo kuokota rambo na plastiki zinazozagaa pembezoni mwa barabara na kufyeka nyasi," alisema.





# Upungufu wa madawati, matundu vyoo shule msingi kufikia tamati

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amesema tatizo la upungufu wa madawati na matundu ya vyoo kwenye shule za msingi katika Jiji la Mbeya litafikia ukomo kabla ya shule hazijafunguliwa Januari 8 mwaka ujao ili wanafunzi wasome katika mazingira rafiki.

Dk. Tulia ambaye ni Rais wa Mabunge Duniani (IPU) aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipofanya mkutano maalumu na mabalozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Jiji hilo pamoja na wenyeviti wa serikali za mitaa. Alisema wanaendelea kupambana na matatizo hayo kwa kuwahimiza mafundi kuongeza kasi ya utengenezaji wa madawati na ujenzi wa miundombinu ya vyoo vya kisasa kwenye shule zilizobakia.

Alisema serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu hasa ujenzi wa vyumba vya madarasa, vyoo na utengenezaji wa madawati. "Hili ndilo Jiji pekee kwa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, sasa hatuwezi tukawa tunajadili tatizo la madawati na vyoo kwenye shule zetu za jiji, hili litakwisha ifikapo Januari watoto wetu watakapokuwa wanafungua shule," alisema Dk. Tulia.

Vilevile alisema wataendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye shule zenye upungufu wa miundombinu hiyo na kukarabati majengo yaliyochakaa ili watoto wote wasome kwenye mazingira yanayofanana.

Alisema serikali kupitia miradi mbalimbali imejenga majengo mapya na ya kisasa kwenye baadhi ya shule na kwamba majengo hayo yamekuwa na tofauti kubwa na yale ya zamani hali ambayo inasababisha shule zisiwe na mwonekano mzuri.

Alisema ukarabati wa miundombinu hiyo utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha pamoja na vipaumbele vya nchi na hivyo akawataka mabalozi na wenyeviti wa serikali za mitaa kuwa wavumilivu na kutoa ushirikiano.

Katika hatua nyingine, Dk. Tulia alisema atagawa misaada ya vifaa vya shule na sare kwa wanafunzi zaidi ya 5,000 wa Jiji hilo wanaotoka kwenye mazingira magumu ili kuwawekea mazingira rafiki ya kuendelea na masomo kama ilivyo kwa wenzao.

Alisema atagawa vifaa hivyo Januari katika shule zote 83 na kwamba atashirikiana na walimu wa shule hizo pamoja na viongozi wa serikali za mitaa kuwachagua watoto wenye sifa za kupatiwa vifaa hivyo.

Akizungumza kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Mjumbe wa Halmashauri Kuu (NEC) Taifa anayewakilisha mkoa huo, Ndele Mwaselala, alisema chama hicho kinaridhika na namna ambavyo Dk. Tulia amekuwa akikiwakilisha.

Alisema chama hicho kitaendelea kumuunga mkono kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo ili azitimize kulingana na alivyopanga na kwamba hawatasita kumshughulikia mtu yeyote atakayekuwa kikwazo.

"Sisi kama chama tunaridhika sana na kazi zako, lakini tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia wewe ukagombee kwenye nafasi ya urais wa mabunge duniani na kuku-



Spika wa Bunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Ackson, akimsikiliza mkazi wa Rungwe nje ya ofisi za Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mbeya Mjini wanaodaiwa kuporwa maeneo yao wilayani humo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## DC, viongozi wilaya kutatua kero za wananchi kwa wakati

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKUU wa Wilaya ya Chunya, Mrakibu Mwandamizi wa Uhamiaji, Mbarak Batenga, amesema atashirikiana na viongozi mbalimbali wa wilaya hiyo kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua kwa wakati ili kupunguza migogoro.

Aidha amesema utatuzi wa haraka wa kero za wananchi utasaidia kuchochea maendeleo kwa kuwa wananchi watatumia muda mwingi kufanya kazi badala ya kulumbana.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa anakabidhiwa ofisi na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Mayeka Simon Mayeka, ambaye amehamishiwa katika Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

"Ukikuta wananchi wanalalamika basi ujuwe sisi viongozi wao hatujatekeleza vizuri majukumu yetu, kwa hiyo nawaomba sana viongozi wenzangu tushirikiane kutatua kero za wananchi, hii ndiyo kazi iliyotuleta huku," alisema Batenga.

Alisema wataandaa utaratibu mzuri wa kusikiliza kero hizo na kuzitatua na kwamba watakuwa wanawafuata wananchi kwenye maeneo yao badala ya wananchi kuwafuata viongozi.

Aliwataka wahandisi wa halmashauri hiyo kusimamia vizuri ujenzi wa miundombinu ya elimu na vituo vya kutolea huduma za afya ili thamani ya fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya miradi hiyo ionekane.

Akizungumza wakati wa kuwaaga watumishi wa wilaya hiyo, Mayeka aliwaomba waendelee kumpatia ushirikiano Betenga kama ambavyo walikuwa wanampatia yeye kwa muda wote aliokuwa anafanya kazi wilayani humo ili wananchi waendelee kupata huduma nzuri.

Alisema ushirikiano uliokuwapo kati ya ofisi yake na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya hiyo, ulisaidia wilaya hiyo kufanya vizuri kwenye miradi mingi ikiwamo vita dhidi ya matatizo ya lishe kwa watoto.

Alisema kwa sasa wilaya hiyo inashika nafasi ya tatu kitaifa kwa kutekeleza vizuri mkataba wa lishe na kwamba walikubaliana kuendeleza juhudi za kuhakikisha wanaendelea kufanya vizuri.

# Wazee 300 wapatiwa misaada sikukuu Krismasi, Mwaka Mpya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya wazee 300 wasiojiweza kutoka katika kata tofauti za mkoani Mbeya, wamepatiwa msaada wa vitu mbalimbali ikiwamo chakula kwa ajili ya sherehe za Krismasi na Mwaka mpya.

Misaada hyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na wafanyakazi wa Shule za Patrick Mission High School ya jijini Dar es Salaam na Paradise Mission Pre and Primary School ya mkoani Mbeya ambao walikuwa wanawafuata wazee hao kwenye maeneo yao.

Akizungumza wakati wa kugawa misaada hiyo, Meneja wa Shule ya Patrick Mission, Peter Msanga, alisema misaada hiyo ni sehemu ya kurudisha kwa jamii faida ambayo imekuwa ikipatikana kutokana na uwekezaji walioufanya.

Alisema waliamua kutoa misaada hiyo kwa wazee kutokana na kundi hilo kutokuwa na uwezo wa kujitafutia na kwamba walishirikiana na viongozi wa kata kuwatafuta wazee wanaostahili kunufaika na msaada huo.

"Tumeamua kutoa msaada huu kwa wazee wetu huku Mbeya kwa sababu mmiliki wa shule hizi ambaye ndiye mwajiri wetu, Ndele Mwaselela anatokea huku na msaada huu hautakuwa mwisho mwaka huu tutaendelea kufanya hivi kila mwaka," alisema Msanga.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Paradise Mission, Rozalina Mtumbuka, alisema walichagua wazee 10 kutoka kwenye kila kata na kwamba wazee hao walikuwa wanachaguliwa na viongozi wa kata husika kwa kuzingatia vigezo walivyopewa.

Alisema moja ya vigezo vilivyotumika kuwachagua wazee hao ni uwezo wa kiuchumi wa familia husika na kwamba wao walikuwa wanakabidhiwa wazee walioteuliwa.

Alisema walilenga kugawa misaada hiyo kupitia ofisi za kata lakini kwenye baadhi ya maeneo walilazimika kuwafuata wazee kwenye makazi yao kutokana na baadhi yao kutokuwa na uwezo wa kutembea kwenda kwenye ofisi za kata.

"Tuligawanyika kwenye makundi matatu na kila kundi lilikabidhiwa kata za kwenda kugawa misaada hii kwa siku nne mfululizo, kuna baadhi ya wazee waliokuwa wameteuliwa walichelewa kufika na hivyo tukakabidhi vitu vyao kwa viongozi wa kata husika ili wawapatie wakifika," alisema Mwalimu Rozalina.

Baadhi ya wazee walionufaika na misaada hiyo waliwashukuru wafanyakazi wa shule hizo wakidai kuwa itawasaidia kusherehekea vizuri sikukuu za krismas na mwaka mpya.

Mmoja wa wazee hao, Yangson Shula wa Kata ya Isuto katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alisema alikuwa hana uhakika wa kusherehekea vizuri na wajukuu zake lakini baada ya kupokea msaada huo matumaini yalifufuka.

Alisema yeye ana wajukuu wanne ambao ni wadogo hawawezi kujitafutia na kwamba huwa anapata tabu kuwalea kutokana na kipato chake kuwa duni.

Mkurugenzi wa shule hizo, ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (NEC) Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, alisema utoaji ni moja kati ya vitu ambavyo huwa anawasisitiza wafanyakazi wake.



# Mfumuko wa bei chanzo hali ngumu maisha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ASKOFU wa Kanisa Katoliki Zanzibar, Augustine Shao, amesema mfumuko wa bei umefanya maisha ya watu kuwa magumu licha ya Serikali ya Zanzibar kufanya juhudi kubwa kuboresha miundombinu ikiwamo barabara, hospitali na masoko.

Akizungumza jana katika ibada ya sikukuu ya Krismasi katika Kanisa Katoliki Shangani visiwani humo, Askofu Shao aliishauri serikali itafute uwezekano wa kupunguza ukali wa maisha kwa kutafuta vianzio vipya vya kufidia bei hizo ikiwamo kuharakisha bima ya afya kwa wote hasa kwa wazee na watoto.

"Asiependa kujinyima kwa ajili yawengine hawezi kuwa kiongozi wa kujenga matumaini ya wananchi maskini kama Tanzania. Mungu Emmanueli alijishusha kwa hali ya watu wake na hivyo akawajengea matumaini," alisema.

Alisema kiongozi makini na mwadilifu ni yule ambaye ni mfano wa uhalisia wa maisha ya watu wake na anayejinyima kwa namna zote ili awafikie wengi anaowaongoza.

"Mafundisho yanasema chochote cha ziada ni mali ya yule uliyemnyima haki yake kwani hakuna utajiri usio shirikisha wengi," alisema.

Alisema kuzaliwa kwa Kristo duniani ni matumaini kwa waovu na Kristo anayesherehekewa ni anayewavutia waovu na wanaodhaniwa kuwa wadhambi ili awainue na kuwapa msamaha.

Hata hivyo alisema Kristo wa sasa ni wa mafisadi wala rushwa, wauza haki za wanyonge kwa faida yao, wanafamilia waliotengana kwa sababu ya uchoyo na udhaifu wa kutosamehe.

"Pia ni Kristo wa walawiti, wa ndoa ya jinsia moja, wanaobadilisha jinsia, wa wale wote wanaoishi kinyume cha maumbile asili ya zawadi ya uumbaji. Hawa wote kristo anawatia na kuwapa matumaini ya kwamba amezaliwa kwa ajili yao na wanachopaswa kufanywa ni kubadilika, kuomba msamaha na kubadilisha misimamo yao," alisema.

Alisisitiza waumini kuwa alama ya matumaini kwa wote wale waliokengeuka maadili ya mafundisho ya injili na kanisa na kuwaombea, kuwasaidia kwa kuwashauri, kuwajumuisha kwa yale mazuri ya kanisa na si kuwanyanyapaa. "Yale mnayosikia Papa Mt. Francis amehalalisha ndoa za jinsia moja na kundi lote la LGTBQ2, lile la Padri au askofu kumbariki mtu wa namna hii siyo kwamba ni mtu anayehitaji msamaha wa Mungu, kamwe baraka ya namna hiyo siyo ibada ya ndoa ambayo ina mwongozo wake ambao ndoa ni mke na mume wenye jinsia mbili tofauti, " alisema.

Alisema kanisa halijahalalisha ndoa za jinsia moja na haliwezi kwenda kinyume cha maagizo ya Mungu na endapo Papa Francis atafanya hivyo umoja wa makardinali na maaskofu watamwondoa kwenye kiti chake kitakatifu.



Waumini wa Kanisa Katoliki Zanzibar wakisali kwenye pango la mtoto Yesu baada ya ibada ya mkesha wa Krismasi iliyofanyika juzi Kanisa la St. Joseph mjini Zanzibar. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

## SMZ kuboresha mazingira biashara

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema itaendelea kuwaweka mazingira mazuri wajasiriamali wadogo ili kufanya biashara zao katika maeneo yaliyobora na yakisasa kwa lengo la kukuza kipato chao na Taifa kwa ujumla.

Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo jana baada ya kuweka jiwe la msingi katika wa mradi wa Soko la Chuini Kwanyanya Wilaya ya Magharibi "A" ikiwa ni mwendelezo wa shamrashamra za kutimia miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema kuwa serikali imeamua kuyajenga masoko hayo kwa kuwaondolea changamoto wafanyabiashara wadogo ili yawanufaishe Wazanzibari na hayuko tayari kuwasaliti kwa kuruhusu makandarasi waliokosa sifa za kujenga miradi mikubwa ya kimaendeleo na kuitia hasara Serikali.

Hemed alisema kwa kipindi kirefu wajasiriamali wamekuwa wakilalamikakutokuwepo maeneo rasmi ya kufanyia biashara zao ambazo zinawasaidia kuwapatia kipato hivyo Serikali itaendelea kuwawezesha kwa kuwapatia mitaji na mikopo nafuu ili kujimudu kiuchumi.

Alisema ni vyema viongozi kuwajibika na kutenda haki kwa kuwatumikia kwa moyo thabit wananchi ili kuunga mkono jitihada za Rais wa Zanzibar, Dk. Hussen Ali Mwinyi ya kuwaletea maendeleo Wazanzibari wote.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara maalum za SMZ, Massoud Ali Mohamed, alisema miongozo inayotolewa na viongozi wakuu wa nchi imechangia soko hilo kufikia hatua nzuri na kuwekewa jile la msingi.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Issa Mahfoudh Haji, alisema mradi wa ujenzi wa Soko la Chuini utajumuisha Soko pamoja na kituo kikuu cha daladala ili kuwaondolea usumbufu wafanyabiashara wa eneo hilo na wananchi wanaofika kupata huduma.

Aidha alisema zaidi ya Sh. bilioni 32 zitatumika hadi kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa Soko hilo na kutoa nafasi kwa wafanyabiashara 2,300 kufanya biashara zao Sokoni hapo na linatarajiwa kutoa ajira kwa watu zaidi ya 5000 kwa wakati mmoja.

Mshauri elekezi kutoka Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA), Shadya Mohd Fauz, alisema mradi wa ujenzi huo umefikia asilimia 75 ambapo kwa sasa upo katika hatu ya kumaliza ili kukabidhiwa kwa Serikali.

# ACT yaja juu zabuni miradi kutotangazwa

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema miradi ya ujenzi inaendelea kuibuka Zanzibar bila ya kutangazwa zabuni kinyume na sheria ya zabuni na manunuzi zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Hayo yameelezwa juzi na Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, alipokuwa akihutubia mkutano wa hadhara katika viwanja vya Daraja bovu madukani uliohudhuriwa na Makamu wa Kwanza wa Rais ambaye ni makamu mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud Othman.

"Kuna jambo linafanyika kimyakimya serikali inataka kuvunja jengo la pili la abiria la Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume na kujenga jengine bila kutangaza zabuni, jambo ambalo halikubaliki katika misingi ya utawala bora," alisema.

Jussa alisema matengenezo ya jengo hilo yanatarajia kutumia dola milioni 30, zaidi ya Sh. bilioni 76 zikiwa ni fedha za umma wakati serikali ilipaswa kutangazwa zabuni na fedha hizo kuidhinishwa matumizi yake na Baraza la Wawakilishi.

"Nimepitia sana vitabu vya bajeti vya mwaka 2023/2024 sikuona sehemu inayozungumzia bajeti ya ujenzi ya jengo la pili la abiri la uwanja wa ndege zaidi ya kuwepo kwa taarifa ya upembuzi yakinifu kuhusu ujenzi wa jengo la abiri la nne katika uwanja huo, lakini hakuna fedha zilizotengwa kwa mwaka huo," alisema.

Aidha alisema kwamba kampuni inayotaka kupewa mradi wa ujenzi huo imewahi kuhusishwa katika Ripoti ya Mkagudhi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa kuzidisha gharama za ujenzi katika miradi ya nyuma za matumizi ya fedha bila ya kuidhinishwa na vyombo husika.

Alisema fedha za kupunguza makali ya athari za kiuchumi yaliotokana na maradhi ya Uviko-19 Sh. bilioni 230 zilizotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Shirika la Fedha Duniani (IMF) hazikutumika vizuri.

Jussa alisema matumizi ya fedha hizo yanakabiliwa na ufisadi mkubwa kwa mujibu wa ripoti ya CAG kupitia miriadi ya ujenzi iliyofanyika Zanzibar, yakiwamo majengo ya hospitali na masoko.

Alisema ujenzi wa masoko ulitengewa karibu Sh. bilioni 75 lakini mpaka sasa karibu bilioni 102 zimeshatumika na masoko hayajakamilika na kusababisha athari kubwa za kiuchumi kwa wananchi wa Zanzibar.

Hata hivyo alisema kuna mkandarasi alishindwa kuendeleza ujenzi wa soko la Mwanakwerekwe huku akiwa amelipwa fedha na serikali kuamua kumnyang'anya kazi lakini hajachukuliwa hatua zozote zak isheria badala yake kazi ya ujenzi wamepewa jeshi la kujenga uchumi (JKU).

Alisema zaidi ya masoko manne yamevunjwa Zanzibar kwa wakati mmoja yakiwemo Mombasa, Jumbi, Mwanakwerekwe na kusababisha mzunguko wa fedha kuathirika katika sekta ya biashara Zanzibar.

# HABARI PICHA



Waumini wa Kanisa la Anglikana Tanzania Dayosisi ya Dar es Salaam wakiwa katika ibada ya Sikukuu ya Krismasi jijini Da es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**





Askofu wa Jimbo Katoliki la Tanga, Mhasham Thomas Kiangio, akizungumza wakati akitoa salamu za sikukuu ya Krismasi katika Kanisa la Mtakatifu Antony wa Paduo jijini Tanga jana. **PICHA: OSCAR ASSENGA**



Watoto wakibembea jana katika viwanja vya Msekwa Park wilayani Muheza, mkoani Tanga, kusherehekea sikukuu ya Krismasi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Wakazi wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, wakipata vinywaji na chakula jana katika kusherehekea sikukuu ya kuzaliwa Yesu Kristo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Askofu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Alex Malasusa, akimbariki mmoja wa waumini wa kanisa hilo wakati wa ibada ya Krismasi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Katibu Mkuu wa Kanisa la KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Julius Madiga, akishiriki ibada ya Krismasi katika kanisa la KKKT Usharika wa Muheza Mjini, mkoani Tanga, akiwa na mke wake Adelina Madiga (kulia). **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Watu 16 wameuawa katika shambulio kaskazini mwa Nigeria

**PLATEAU,** NIGERIA

JESHI la Nigeria limesema watu 16 wameuawa katika shambulio kaskazini mwa nchi hiyo ambako mapigano kati ya wafugaji na wakulima yanatajwa kuwa ni ya kawaida.

Kapteni Oya James alibainishwa kuwa shambulio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Jumamosi katika kijiji cha Mushu kwenye jimbo la Plateau.

Inaelezwa kuwa eneo hilo liko kwenye mstari unaoligawa eneo kati ya Waislam walio wengi huko kaskazini na Wakristo wa kusini nchini Nigeria na kwamba kwa miaka mingi wamekuwa wakikabiliwa na mivutano ya kikabila na kidini. Licha kwamba haikufafanuliwa mara moja kile kilichosababisha shambulio hilo na nani aliyehusika.

Maofisa wa usalama walipelekwa kuzuia mapigano zaidi katika eneo hilo, ambako mauaji ya kulipiza kisasi, kati ya wafugaji ambao mara nyingi ni Waislamu na wakulima ambao kwa ujumla ni Wakristo, na kwamba mara kwa mara hugeuka kuwa mashambulizi ya kijiji yanayofanywa na magenge yenye silaha.

Gavana wa Jimbo hilo, Caleb Mutfwang, alilaani shambulio hilo akieleza kuwa ni la kikatili na halikuwa na maana na kuapa kuwafikisha wahusika katika vyombo vya sheria. **VOA**

**Kapteni Oya James alibainishwa kuwa shambulio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Jumamosi katika kijiji cha Mushu kwenye jimbo la Plateau.**

# Papa ahimiza amani vita vikitia dosari Krismasi

**VATICAN,** ROMA

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, amewakumbusha waumini kuhusu umuhimu wa amani, baada ya sikukuu ya Krismasi kuonekana kutiwa dosari kutokana na vita vinavyoendelea huko Ukanda wa Gaza na Ukraine.

Papa Francis alitoa wito huo jana wakati wa ibada ya Krismasi Mjini Vatican, ambayo inakumbuka kuzaliwa kwa Yesu Kristo miaka 2000 iliyopita.

Kwenye mahubiri yake Papa Francis alisema "mioyo yetu iko Bethlehem, ambako mwanamfalme wa amani kwa mara nyingine amekataliwa kwa kushamiri kwa vita, mapigano ya kutumia silaha ambayo hata leo yanamzuia kupata nafasi ulimwenguni".

Kiongozi huyo aliongeza kuwa kichwani mwake anauwaza umma unaoteseka kwa vita huko Palestina, Israel na Ukraine.

Aidha, ilielezwa kuwa mjini Bethlehem inakoaminika Yesu Kristo alizaliwa zaidi ya miaka 2000 iliyopita, sherehe za kila mwaka za Krismasi zimefutwa ikiwa ni pamoja na shamrashamra na mapambo ya mji mzima ambayo huwavutia maelfu ya watalii, huku sababu ikitajwa kuwa ni kutokana na machafuko yanayosababisha vifo vya watu.

Hata hivyo ilibainishwa kuwa hakukuwa na mti mkubwa wa Krismasi ambao huwekwa kila mwaka kwenye mji huo wala maandamano ya vikundi vya kwaya na muziki. Na kwamba mji huo ulishuhudiwa ukiwa umepooza huku taa chache zikionekana zimetundikwa kuashiria msimu wa Krismasi.

Katikati mwa mji huo uliopo eneo la Ukingo wa Magharibi, bendera kubwa ya Palestina ilitandazwa juu ya bango lenye ujumbe unaosomeka "kengele za Bethlehem zinagongwa kuhimiza usitishaji mapigano Ukanda wa Gaza".

Mwanafunzi wa miaka 18 Nicole Najjar, alipozungumza na Shirika la Habari la AFP alisema "Watu wengi wanakufa kwenye ardhi hii, ni ngumu kusherehekea wakati watu wetu wanakufa."

Ilielezwa kuwa nchini Syria, makanisa yamepunguza shamra shamra na badala yake yameamua kufanya ibada kuonesha mshikamano na Wapalestina.

Huko Ukraine, ambako Russia iliivamia karibu miaka miwili iliyopita, watu wanasherehekea Krismasi kwa mara ya kwanza, ikiwa ni hatua ya kujitenga na ile ya Januari 7 chini ya madhehebu ya Orthodox. Ilibainishwa kuwa mabadiliko hayo ni sehemu ya juhudi kubwa za nchi hiyo kujitenga na ushawishi na urithi wa Russia.

Pia Kusini mwa Uturuki, sehemu kubwa ya eneo hilo iliharibiwa na tetemeko la ardhi la mnamo Februari na kwamba waumini walisherehekea misa ya mkesha kwenye mabaki ya kanisa huko Antakya.

"Ni muhimu kwetu kusherehekea kuzaliwa Yesu Kristo, lakini ni Krismasi ya huzuni sana," amesema Vehbi Tadrasgil, mwenye umri wa miaka 55 ambaye anatajwa kupoteza mke na watoto wake wawili katika tetemeko la ardhi lililowaua takribani watu 50,000 nchini humo na zaidi ya 50,000 nchini Syria.



Wanajeshi wa Ukraine wakihudhuria sherehe ya Krismasi, licha ya Russia kufanya shambulio huko Lviv, jana.
**PICHA MTANDAO**

# Askofu Ambongo ang'aka uchaguzi DRC

## •Adai uligubikwa na mgogoro

**KINSHASA,** DRC

ASKOFU Mkuu wa Kinshasa, Kardinali Fridolin Ambongo, ametoa wito wa utulivu kwa jamii, huku akionyesha kutoridhishwa na kile alichoelezea kama vurugu kubwa katika uchaguzi mkuu wa nchini humo uliofanyika wiki iliyopita.

Alitoa wito huo jana akihutubia katika ibada ya sikukuu ya Krismasi, wakati taifa hilo likigubikwa na wimbi la uchaguzi, huku wagombea kadhaa wa upinzani wakitangaza dhamira ya kufanya maandamano Desemba 27, mwaka huu kwa madai kwamba uchaguzi huo haujakizi vigezo.

"Kwa shauku, kwa dhamira, wengi wetu tulijitokeza kidemokrasia kuelezea chaguo letu. Lakini kile kilichopaswa kuwa sherehe kubwa ya maadili ya kidemokrasia haraka iligeuka na kuwa hali ya watu wengi kuchanganyikiwa," alisema.

"Uchaguzi ulikuwa wenye mgogoro mkubwa wa kupangwa, na nyote nyie ni mashahidi wa jambo hili. Tunatoa taswira gani ya nchi yetu duniani? Tunawezaje kuwa na tabia chafu zisizovumilika kama hizi?" Alihoji Askofu Ambongo.

Aidha, katika uchaguzi huo Rais wa DRC anayemaliza muda wake, Félix Tshisekedi, anawania muhula wa pili dhidi ya wagombea wengine 18, ambao baadhi yao wameshutumu machafuko na makosa ambayo wanaamini yaliharibu uchaguzi, huku wengine wakitaka uchaguzi ufutwe.

Miongoni mwa wapinzani hao ni pamoja na Moïse Katumbi, gavana wa zamani wa mkoa wenye madini wa Katanga Kusini Mashariki, Martin Fayulu, ambaye anadai ushindi uliibiwa kutoka kwake katika uchaguzi wa mwaka 2018.

Mwingine ni Denis Mukwege, mshindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel kwa huduma yake aliyoitoa kwa waathiriwa wanawake waliobakwa wakati vita vilikuwa vikipamba moto nchini DRC.

Hata hivyo kutokana na matatizo mengi ya vifaa, muda wa kupiga kura uliongezwa na tume ya uchaguzi (CENI). Na kwamba uchaguzi huo ulimalizika rasmi Alhamisi jioni lakini uliendelea hadi wikiendi katika mikoa kadhaa.

"Kwa sasa, ninawaomba muwe waangalifu na wenye kujizuia. Tunasubiri ripoti kutoka kwa jumbe mbalimbali za waangalizi, hasa ile ya misheni ya pamoja ya Kanisa Katoliki na Kanisa la Kiprotestanti, ambayo inaweza kutusaidia kutathmini dosari zilizojitokeza na kutathmini athari zake katika uaminifu wa chaguzi hizi," alisisitiza.

**RFI, VOA**

# MATAMPI, YONA WAMFUNIKA DIARRA 'CLEAN SHEETS' BARA

Na Adam Fungamwango

GOLIKIPA wa Coastal Union, Ley Matampi na Yona Amosi anayedakia Tanzania Prisons wanaongoza kwa kucheza mechi nyingi bila kuruhusu nyavu zao kutikishwa katika Ligi Kuu Bara hadi kufikia mechi za raundi ya 14, imefahamika.

Makipa hao wamecheza mechi sita kila mmoja bila kuruhusu wavu wao kuguswa 'clean sheets', ikiwa ni idadi kubwa ya magoli kipa kukaa langoni bila kuruhusu bao.

Kwa mujibu wa dawati letu la takwimu, Matampi ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo (DRC), alisajiliwa na timu hiyo akitokea Renaissance ya nchini kwao huku Yona akiwa ni kipa wa muda mrefu wa Wajelajela hao.

**Magolikipa hao wamewazidi makipa wengi wenye majina na wanaochezea timu kongwe hapa nchini, ambazo ziko juu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Wakati Matampi akiongoza kwa 'clean sheets', timu yake ya Coastal Union ipo katika nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 19 baada ya kucheza michezo 14 mpaka sasa.

Yona ambaye ni Mtanzania, anabebwa na takwimu za 'clean sheets' lakini timu yake ipo katika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa na pointi 17 baada ya kushuka dimbani katika michezo 14.

Wanaoshika nafasi ya pili kwa 'clean sheets' katika ligi hiyo inayotoa wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika ni Djigui Diarra wa Yanga, Constantine Malimi wa Geita Gold na John Noble wa Tabora United ambao kila mmoja amecheza mechi tano bila kuruhusu goli.

Diarra ambaye ni raia wa Mali ameiongoza timu yake kukaa katika nafasi ya pili kwenye msimamo wakati Noble ni Mnigeria na Malimi akiwa ni mzawa.

Golikipa mkongwe, raia wa Burundi, Johathan Nahimana wa Namungo FC anakamata nafasi ya nne kwa 'clean sheets' akikaa langoni bila kuruhusu bao mara nne.

Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayotarajia kufanyika Zanzibar kuanzia kesho pamoja na Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON), zitakaoanza mapema Januari nchini Ivory Coast.



Waimbaji wa Kwaya ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Azania Front jijini Dar es Salaam wakiimba wakati wa Ibada ya Sikukuu ya Krismasi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Lusajo anukia Azam, Singida

Na Adam Fungamwango

STRAIKA tegemeo wa Namungo FC, Reliants Lusajo, ametangaza kuachana na timu hiyo na kusema anahitaji kwenda kupata changamoto mpya, imefahamika.

Ingawa hajaweka wazi wapi anakwenda, taarifa zilizopatikana zinasema straika huyo anawindwa na Singida Fountain Gate FC pamoja na Azam, katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Timu hizo mbili zinatajwa kuhitaji huduma ya Lusajo katika mipango ya kuongeza nguvu katika safu ya ushambuliaji.

"Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi mzima wa Namungo na benchi la ufundi bila kusahau mashabiki wote wa timu hiyo kwa kipindi chote tulichokua pamoja, ni muda wangu sasa wa kuangalia changamoto sehemu nyingine, nipende kuwatakia kila la kheri katika msimu huu wa ligi," alisema mchezaji huyo ambaye amefunga mabao mawili msimu huu.

Hata hivyo viongozi wa Namungo bado hawajasema lolote kuhusu uamuzi wa mshambuliaji huyo ambaye anatajwa amemaliza mkataba na timu hiyo ya mkoani Lindi.

Lusajo ambaye aliwahi kuichezea timu ya Taifa ya Tanzania ( Taifa Stars) ni mmoja wa mastraika wachache Watanzania ambao wana uwezo wa kupachika mabao angalau 10 kwa msimu mmoja, alianza kujulikana akiwa na kikosi hicho tangu mwaka 2020.

Nyota huyo pia aliwahi kuitumikia KMC, lakini akarejea tena Namungo katika mzunguko wa pili wa msimu wa 2020/21 hadi jana alipotangaza kuachana na timu hiyo.

# Bandari, Warriors Queens kuumana

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Bandari Queens itakutana na Warriors Queens katika mechi ya ufunguzi ya mashindano ya netiboli ya kuwania ubingwa wa Kombe la Mapinduzi 2024 itakayochezwa Januari 4, mwakani kwenye Uwanja wa Gymkhana Visiwani hapo.

Mashindano hayo yanatarajiwa kushirikisha timu sita, zote zikitoka Kisiwani Unguja ambazo ni JKU, Zimamoto, Mafunzo, KVZ, Bandari na Warriors.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Netiboli Zanzibar (CHANEZA), Said Mansab, alisema maandalizi ya mashindano hayo yamekamilika na kuongeza mwaka huu hakuna timu zitakazoshiriki kutoka nje ya Zanzibar.

Alisema kukosekana kwa wadhamini ndio sababu ya kushindwa kualika timu kutoka nje ya Zanzibar kama ilivyo kawaida yao na kuwaomba wadau kuuangalia mchezo huo kama wanavyoongeza nguvu katika mpira wa miguu.

"Mwaka huu tunakabiliwa na shughuli mbalimbali ikiwamo kuandaa uchaguzi, tunasikitika tumeshindwa kuwaalika wenzetu kutoka Kenya ambao walikuwa tayari kuja kushindana," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kwa kuwaomba wadau wa michezo kujitokeza kushuhudia vipaji vya wachezaji wao ambao wameahidi kuonyesha viwango bora.

Kwa upande wa soka, mapingwa watetezi Mlandege wanatarajia kufungua pazia la michuano hiyo keshokutwa kwa kuvaana na URA kutoka Uganda kuanzia saa 10:15 jioni na baadaye usiku Chipukizi itawaalika Azam FC.

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wao wataanza kampeni za kuwania taji hilo Desemba 31, mwaka huu kwa kucheza dhidi ya Bandari FC kutoka Kenya wakati Januari Mosi, mwakani Jamhuri itawakaribisha Simba.

Fainali za mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka zitafanyika Januari 13, mwakani na bingwa atajinyakulia kitita cha Sh. milioni 100 huku mshindi wa pili akiondoka na Sh. milioni 70.

## ZISIKUPITE

### CITY YAMTAKA ECHEVERRI

KLABU ya Manchester City inaendeleza mazungumzo kuhusu kumnunua kiungo wa River Plate mwenye umri wa miaka 17, Claudio Echeverri, huku Chelsea pia ikimtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina. (***Fabrizio Romano***)

### BARCELONA, CITY VITANI

BARCELONA inakabiliwa na ushindani kutoka kwa Manchester City kuwania saini ya kiungo wa Fluminense, Andre (22), huku Pep Guardiola, akimtambua Mbrazil huyo ambaye anahusishwa na Liverpool na Fulham, kama mchezaji anayetarajiwa kusajiliwa kwa siku zijazo. (***Mundo Deportivo***)

### WACHEZAJI WATAKIWA EPL

KLABU za Ligi Kuu England zinatazamiwa kukabiliwa na wimbi jipya la kutaka kuwanunua wachezaji wao wakuu kutoka Ligi Kuu ya Saudia huku idadi ya nyota wa kigeni inayoruhusiwa katika vikosi vyao kuongezeka kutoka nane hadi 10. (***Daily Telegraph***)

### KIMMICH AKARIBIA UNITED

KLABU ya Manchester United imeungana na Manchester City na Liverpool katika mbio za kumsajili kiungo wa Ujerumani, Joshua Kimmich, mwenye umri wa miaka 28 kutoka Bayern Munich. (***Fichajes***)

### ARSENAL KUMUUZA NKETIAH

ARSENAL iko tayari kumuuza mshambuliaji wa England, Eddie Nketiah, mwenye umri wa miaka 24 kwa ada ya takribani pauni milioni 40 huku West Ham, Brentford na Crystal Palace zikimwania nyota huyo. (***Football Insider***)

### CONTE ATAJWA MILAN

AC Milan inabakia na Kocha Stefano Pioli, kwa wakati huu, licha ya mwalimu wa zamani wa Chelsea na Tottenham Hotspur, Antonio Conte, kuonekana kama anafaa kuwa mbadala wa msimu ujao. (***Gazetta dello Sport***)

### CHERKI ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United imemweka kiungo mkabaji wa Lyon, Rayan Cherki, mwenye umri wa miaka 20 kwenye orodha ya wachezaji wanaotakiwa na timu hiyo. (***Football transfer)***

### CANCELO ATOLEWA RASMI

KLABU ya Manchester City inaitaka Barcelona kulipa zaidi ya pauni milioni 26 ili kufanya uhamisho wa mkopo wa mlinzi wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Cancelo, kubadilika na kusajili wa kudumu. (***Sport)***

### OSIMHEN HAONDOKI NAPOLI

WAKALA wa mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 24 amepuuza tetesi kuhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria ataondoka katika klabu hiyo msimu ujao. (***Corriere dello Sport)***

### DIALLO RUHUSA KUONDOKA

KLABU ya Manchester United iko tayari kumruhusu winga wa Ivory Coast, Amad Diallo, kuondoka Old Trafford kwa mkopo ifikapo Januari, huku Southampton wakimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. (***Football Insider***)

### BERALDO KUTUA PSG

KLABU ya Paris St-Germain imekubali ada ya pauni milioni 17.5 na Sao Paulo kwa ajili ya beki wao wa kati Mbrazil, Lucas Beraldo mwenye umri wa miaka 20 ambaye pia alikuwa kwenye rada za bosi wa Liverpool, Jurgen Klopp. (***L'Equipe***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RATCLIFFE, UNITED SASA KIMEELEWEKA

**MANCHESTER,** England

**●●● Ni mchakato wa uwekezaji wa klabu hiyo ambapo...**

MANCHESTER United imethibitisha imekubali kuuza hisa chache kwa Sir Jim Ratcliffe, huku mwenyekiti huyo wa INEOS pia akijitolea kuwekeza Dola za Marekani milioni 300 katika klabu hiyo.

Ratcliffe amepata asilimia 25 ya hisa katika klabu hiyo kwa mkataba wenye thamani ya pauni bilioni 1.3 na pia atawajibika kwa uendeshaji wa soka katika United.

**Taarifa iliyotolewa juzi ilisema ahadi yake zaidi ya Dola milioni 300 "inakusudiwa kuwezesha uwekezaji wa siku zijazo Old Trafford."**

"Kama mshabiki wa klabu kwa muda mrefu, nimefurahishwa sana, tumekubaliana na Bodi ya Manchester United ambayo inatukabidhi jukumu la usimamizi wa shughuli za soka za klabu," alisema Ratcliffe katika taarifa yake.

"Ingawa mafanikio ya kibiashara ya klabu yamehakikisha kila mara kumekuwa na fedha za kushinda mataji kwa kiwango cha juu, uwezo huu haujafunguliwa kikamilifu katika siku za hivi karibuni.

"Tutaleta maarifa ya kimataifa, utaalamu na talanta kutoka kwa kundi pana la INEOS Sport ili kusaidia kuboresha zaidi katika klabu, huku pia tukitoa fedha zinazokusudiwa kuwezesha uwekezaji wa siku zijazo hapa Old Trafford.

"Tupo hapa kwa muda mrefu na tunatambua kuna changamoto nyingi na kazi ngumu mbele yetu, ambayo tutakabiliana nayo kwa ukali, weledi na mapenzi. Tumejitolea kufanya kazi na kila mtu katika klabu, bodi, wafanyakazi, wachezaji na mashabiki, kusaidia kuipeleka klabu mbele.

"Matarajio yetu ya pamoja yako wazi: Sote tunataka kuiona Manchester United ikirejea pale tunapostahili, katika kilele cha soka la Uingereza, Ulaya na duniani."

Ratcliffe atapata asilimia 25 ya hisa za Daraja B za klabu, ambazo hapo awali zilikuwa zikishikiliwa na familia ya Glazer pekee, na hadi asilimia 25 ya hisa za Daraja A, ambazo zinauzwa katika soko la hisa la New York.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN viti viwili kwenye bodi ya soka vitaenda kwa Sir Dave Brailsford na Jean-Claude Blanc.

"Tuna furaha kukubaliana mkataba huu na Sir Jim Ratcliffe na INEOS," wenyeviti wenza na wakurugenzi Avram Glazer na Joel Glazer walisema katika taarifa hiyo.

"Kama sehemu ya ukaguzi wa kimkakati tuliotangaza mnamo Novemba, mwaka 2022, tulijitolea kuangalia njia mbadala za kusaidia kuimarisha Manchester United, tukilenga kuleta mafanikio kwa timu zetu za wanaume, wanawake na Academy."

# MO SALAH AIONYA LIVERPOOL




**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah ameionya Liverpool "haiwezi kuendelea kupoteza pointi" katika mbio za ubingwa baada ya kupoteza dhidi ya Arsenal na Manchester United kwenye Uwanja wa Anfield.

Bao la mapema la Gabriel lilifutiliwa mbali na Mohamed Salah, licha ya wote kushinikiza ushindi, timu mbili bora za Ligi Kuu England ziliambulia pointi moja.

Ilikuwa ni sare ya pili mfululizo ya Liverpool nyumbani katika Ligi Kuu England, kufuatia sare ya bila kufungana na Manchester United.

Salah aliandika kwenye mtandao wa X: "Tunajua hatuwezi kuendelea kuangusha pointi kama hii na tutaendelea kupambana kufanya vizuri zaidi."

Arsenal walisawazisha tena uongozi wa juu kileleni katika Ligi Kuu England wakati wa Krismasi lakini wakiondoka na ushindi kwenye Uwanja wa Anfield kumeendelea hadi mwaka wa 12 baada ya sare ya 1-1 iliyoihakikishia Liverpool kuendelea na kasi katika mbio za ubingwa.

Kuwa vinara hadi Desemba 25 sio hakikisho la utendaji wa siku zijazo, hata hivyo, kwani klabu zote mbili zinafahamu vyema; katika mara sita zilizopita timu imeshindwa kuendelea na kunyanyua kombe kutoka nafasi hii ilikuwa mojawapo.

Jamie Carragher anaamini kuna kitu kibaya na safu ya mbele ya Liverpool na akapendekeza Jurgen Klopp akahitaji kusajili mbadala wa Luis Diaz.

# Arteta: Nitaongeza nguvu kikosi changu



**LONDON,** England

MIKEL Arteta ameweka bayana namna Arsenal watakavyoonekana kuimarika mwaka 2024, akisisitiza washikabunduki hao wanahitaji kufanyia kazi mapungufu yao.

Shukrani kwa sare yao dhidi ya Liverpool hapo juzi, Arsenal wapo kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu England, ikiwa na Krismasi nzuri kwa msimu wa pili mfululizo, pointi moja zaidi ya Liverpool na Aston Villa.

Baada ya kupoteza uongozi wao kwa Manchester City msimu uliopita, Arteta na wenzake. watatafuta kuimarika kuhifadhi nafasi yao ya sasa kwenye kilele hadi mwisho wa kampeni wakati huu.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu jinsi Arsenal inavyoweza kufanya hivyo, Arteta aliashiria maeneo machache ambayo timu yake inaweza kuimarika.

"Kuna baadhi ya mambo inabidi tuboreshe ili kuendelea na ubabe tunaoonyesha," alisema Arteta.

"Wakati mwingine matokeo yamekuwa karibu sana, ambapo imetubidi kuchimba katika dakika chache zilizopita ili kudumisha matokeo na ndivyo hivyo, hakuna kingine.

"Natumai tumedumisha kiwango hicho tukiwa na wachezaji watano muhimu nje kwa sababu tumepoteza wachezaji watano muhimu sana kwetu kwa miezi mingi sana na timu bado imeonyesha hivyo hivyo ni jambo ambalo tunatakiwa kulidumisha, ni ubora wa hali ya juu."

Arteta pia alijadili jinsi Arsenal ilivyoimarika tayari wakati wa kampeni za 2023/24, akiashiria "ukomavu" ulioonyeshwa kwenye sare kwenye Uwanja wa Anfield hapo juzi kama uthibitisho.

Aliongeza: "Hakika wamepata uzoefu zaidi na ulikuwa mchezo tofauti sana na mwaka jana."

Arsenal watarejea uwanjani keshokutwa watakapowakaribisha West Ham United kwenye Uwanja wa Emirates.

# Pochettino afunguka wanatakiwa kujilaumu

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino amesisitiza Chelsea "ni adui yetu wenyewe na tunatakiwa kujilaumu wenyewe" baada ya kufungwa 2-1 na Wolves hapo juzi, - huku kocha huyo wa The Blues akisikitikia timu yake kutokuwa na umaliziaji mzuri.

Mario Lemina na Matt Doherty waliwafungia wenyeji katika mechi ya mkesha wa Krismasi, kabla ya Christopher Nkunku kuifungia Chelsea bao katika mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu England uliochezwa kwenye Uwanja wa Molineux.

Chelsea walilazimishwa kulipa kwa kukosa nafasi kadhaa za kufunga na Pochettino anasema timu yake 'inastahili zaidi' lakini wanaweza kujilaumu kwa kupoteza.

"Tulifanya makosa. Tunapaswa kujilaumu wenyewe. Ndio maana hatukushinda. Tulipata nafasi za kufunga," alisema Pochettino.

"Sisi ni adui zetu wenyewe. Leo (juzi), tumepoteza mchezo. Tunajisikia kukata tamaa sana kwa sababu nadhani tunastahili zaidi. Shindano hili linakuumiza wakati hauko na uwezo mzuri wa kumalizia. Tumeunda nafasi. Ndio maana inakatisha tamaa. Tulikubali baada ya kona chache na ilikuwa ngumu sana."

Chelsea wamekosa nafasi nyingi zaidi katika Ligi Kuu England msimu huu, kulingana na Opta.

Pochettino aliangazia vijana wa kikosi chake cha sasa kama sababu ya kushindwa kwa Chelsea kuwa katika nafasi ya tatu kutoka mwisho.

"Tulizungumza sana mwanzoni mwa msimu. Sisi ni vijana kwa umri. Ni timu changa," alisema Pochettino.

"Tuna wachezaji wanaocheza kwa mara ya kwanza kwenye ligi. Wanahitaji kukabiliana. Ni kujiamini na kuhusu ubora.

"Tunahitaji kufunga ikiwa tunataka kushinda mechi. Tumekata tamaa sana. Wakati mwingine inabidi tuwe na bao safi ikiwa hatuwezi kufunga. Tulikubali kona nyingi sana. Tunahitaji kuendelea na kusukuma. Timu za vijana hujifunza kutokana na aina hii ya mchezo.'



HABARI MICHEZO

# KOCHA SINGIDA FOUNTAIN GATE ABWAGA MANYANGA

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Singida Fountain Gate FC, Ricardo Ferreira, ameamua kuachana na timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa imepita siku chache baada ya timu hiyo kupoteza mechi dhidi ya Geita Gold FC ya mkoani Geita, imefahamika.

Taarifa zilizopatikana jijini zinasema Ferreira ameamua kubwanga manyanga kutokana na kukataa kufuata maelekezo ya viongozi wake ya kupanga wachezaji ambao ametakiwa kuwatumia.

Chanzo chetu kilisema Ferreira alifikia uamuzi huo tangu Ijumaa iliyopita na sasa anajiandaa kwenda Singida kuchukua vitu vyake na baadaye kuanza maandalizi ya kurejea nchini kwao.

"Kulitokea sintofahamu kati ya viongozi na kocha huyo kwa sababu ya kutotaka kubadili wachezaji ambapo Ferreira hakutaka kukubaliana na uamuzi huo na hatimaye kuamua kuachana na timu hiyo," kilisema chanzo chetu.

Chanzo hicho kiliongeza baada ya kujiondoka katika kikosi, sasa benchi la ufundi la timu hiyo litakuwa chini ya Kocha Msaidizi, Thambo Senong.

"Mabosi wameamua kumpa Kocha Msaidizi (Thambo) jukumu la kuiongoza timu kuelekea Visiwani Zanzibar katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi," kiliongeza chanzo chetu.

Nipashe lilimtafuta Ofisa Habari wa Singida Fountain Gate, Hussein Massanza, alisema kwa sasa nguvu na akili zao ni kujiandaa na mashindano ya kuwania ubingwa wa Kombe la Mapinduzi na watapelekea kikosi kamili katika michuano hiyo.

Massanza alisema wanahitaji kufanya vyema katika mashindano hayo na watatumia muda huo kukijenga kikosi kwa ajili ya kumaliza kuingia katika duru la lala salama la Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa imara.

"Tutaenda katika Mashindano ya Kombe la Mapinzudi tukiwa 'full mkoko' kama ilivyokuwa msimu uliopita, tutasafiri baada ya Krismasi, kwa maana hiyo Jumatano tutakuwa Zanzibar panapo majaliwa, tunakwenda kupambana kuchukuwa kombe.

Mashindano haya kila siku yanakuwa na ushindani, ubora wake unaongezeka, ubora wa michuano yoyote ni ile hali ya ushindani, Serikali ya Zanzibar inajitahidi sana kuikuza michuano hii kila mwaka," alisema Massanza.

Aliongeza ongezeko la timu za nje ya Tanzania unaifanya michuano kuwa migumu na yenye ushindani, lakini inasaidia kuimarisha timu zao kuelekea mzunguko wa pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema pia klabu hiyo inaendelea kujipanga kuhakikisha wanamalizana na aliyekuwa beki wao, Pascal Wawa, ili wamalize adhabu ya kufungiwa kusajili waliopewa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).



Bondia Twaha Kiduku (katikati), akimpa zawadi mpinzani wake Mganda Mohamed Sebyala (kulia). Mabondia hao wanatarajia kukutana katika pambano la usiku wa Boxing on Boxing Day litakalofanyika leo kwenye Ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# *Kilimanjaro Stars yawasili Zanzibar*

Na Saada Akida

TIMU ya Soka ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), imewasili salama Zanzibar tayari kwa ajili ya mchezo wa kirafiki dhidi ya wenyeji Zanzibar Heroes utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Amaan, visiwani humo.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema kikosi hicho chenye wachezaji 25 kimeanza kambi rasmi jana na benchi la ufundi linatarajia kutumia mchezo huo kama sehemu ya maandalizi ya kuelekea katika Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON).

Ndimbo alisema baada ya mchezo huo timu itabakia Zanzibar hadi mwisho wa mwezi huku wakisubiri kukamilisha kwa safari ya kuelekea Algeria ili kuendelea kujiimarisha.

"Kikosi chetu kimeshaingia kambini na kinaondoka leo (jana) kuelekea Zanzibar kucheza mechi ya kirafiki na baada ya hapo timu itasafiri kwenda nje ya nchi kuendelea na maandalizi ya utulivu kuelekea fainali za AFCON zitakazofanyika mapema mwakani," alisema Ndimbo.

Aliongeza bado TFF iko katika hatua za mwisho za mazungumzo ya kupata timu itakayocheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Taifa Stars.

Wachezaji walioingia kambini chini ya Kocha Mkuu, Adel Amrouche, ni Kwesi Kawawa kutoka Karilsud IF - Sweden, Beno Kakolanya, Yusuf Kagoma (Singida Fountain Gate, Aishi Manula (Simba), Bakari Mwamnyeto, Nickson Kibabage, Dickson Job (Yanga), Lusajo Mwaikenda na Sospeter Bajana wa Azam.

Wengine ni Israel Patrick, Mzamiru Yassin, Mohammed Hussein, Kibu Denis (Simba), Edwin Balua (Prisons), Ladeki Chasambi (Mtibwa Sugar), Adam Kasa (Ifk Haninge - Sweden), Zion Nditi (Alderson Town - England, Mark John (Kingston FC - Australia), Miano Danilo ( Villena CF - Hispania), Adolf Bitegeko (Volsungur IF- Iceland), Robert Yohana (Fofar Athletic - Scotland, Said Hamis (Jedinstov UB - Serbia) Tarry Allarakhia (Wealdstone - England) na Simon Msuva anayekipiga Morocco.

## *Bingwa Mapinduzi Cup kupata 100m/-*

INATOKA UK 24

kwa ajili ya kuanza maandalizi ya kuelekea kwenye fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON), zitakazofanyika kuanzia Januari 13 hadi Februari 11, mwakani nchini Ivory Coast.

## Simba SC, Yanga zaandaa 'suprise'

INATOKA UK 24

Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, nyingine zinaendelea na nyingine zimetolewa.

Lakini kwa sasa ni lazima utumie pesa nyingi sana na anaweza kuja kupindi hiki pia asifanye chochote kwa sababu hajui mazingira, nchi, mfumo na vitu vingine, ila tutajitahidi," alisema kocha huyo.

Baadhi ya washambuliaji wanaotajwa kuwindwa na Yanga ni Sankara Karamo wa Asec Mimosas ya Ivory Coast na Emmanuel Bola anayecheza FC Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Jonathan Sowah wa Medeama ya Ghana.

Taarifa zinasema ada ya uhamisho ya Bola kujiunga na Yanga inatajwa kuwa ni Dola za Marekani 100,000 lakini kumekuwa na sintofahamu kuhusu nyota huyo kuridhia kujiunga na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tayari Gamondi alishawaambia aina ya mshambuliaji anayemhitaji na kilichobakia ni kukamilisha masuala machache, baada ya hapo watamtambulisha ili kujiunga mazoezini mapema kwa ajili ya kujiandaa na michuano mbalimbali inayowakabili," kilisema chanzo chetu.

Naye Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema kikosi chao kinakwenda Zanzibar kikiwa kimesahau matokeo ya mechi zilizopita kwa sababu wanahitaji 'kuzaliwa' upya.

Ahmed alisema watatumia mashindano hayo kuongeza ubora wa wachezaji wao lakini kupambana kuwania taji la michuano hiyo yenye historia kubwa nchini.

"Tutashiriki katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi tukiwa kamili, ukiondoa nyota ambao wanakwenda kutumikia mataifa yao, tunahitaji heshima," Ahmed alisema.

# Michezo

Jumanne Desemba 26, 2023

Nipashe




Ratcliffe, United kimeeleweka UK. 21



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), wakiwa bandarini tayari kuelekea Zanzibar kwa ajili ya mechi ya kirafiki dhidi ya wenyeji (Zanzibar Heroes), itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Amaan. **PICHA: TFF**

# Bingwa Mapinduzi Cup kupata 100m/-

## ●●●Zawadi pia zaongezwa kwa tuzo ya Mfungaji Bora, Mchezaji Bora na...

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BINGWA wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa mwaka 2024 atajinyakulia kitita cha Sh. milioni 100 wakati timu itakayomaliza katika nafasi ya pili itazawadiwa Sh. milioni 70, imeelezwa.

Mlandege FC ya Zanzibar ndio mabingwa watetezi wa michuano hiyo inayofanyika kila mwaka ambapo alipokea zawadi ya Sh. milioni 50.

Mashindano ya Kombe la Mapinduzi mwaka huu yatafanyika kuanzia keshokutwa hadi Januari 13, mwakani na yanadhaminiwa na Azam Media, NMB, PBZ pamoja na wadhamini wengine wadogo wadogo.

Akizungumza jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kombe la Mapinduzi, Mbarouk Othman, alisema kuongezeka kwa zawadi hizo kumetokana na jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Michezo.

Othman alisema pia kutakuwa na zawadi kwa Mchezaji Bora wa kila mechi, Mfungaji Bora, Kipa Bora na Mchezaji Bora wa mashindano hayo.

Alisema wanatarajia ushindani katika mashindano ya mwakani itaongezeka kutokana na kuongeza idadi ya timu kutoka nje ya Zanzibar na wanaamini kila upande utapambana kuwania ubingwa wa michuano hiyo.

"Katika kuhakikisha tunaendelea kuboresha mashindano haya, tumeona ipo haja ya kuendelea kuongeza zawadi kwa bingwa na zawadi nyingine kwa tuzo zile ndogo ndogo ili timu zipate ari ya kupambana kwa hali ya juu," alisema Othman.

Aliongeza kamati yake imefanya mabadiliko madogo katika ratiba na uamuzi huo umetokana na timu mbili kujitoa katika mashindano kwa sababu zao binafsi.

"Timu zilizojitoa ni Bandari FC kutoka Kenya na URA ya Uganda, lakini tayari nafasi zao zimechukuliwa na JKU ya Zanzibar pamoja na Jamus kutoka Sudan Kusini," Othman alisema.

Alizitaja timu kutoka nje ya Tanzania ambazo zitashiriki katika michuano hiyo ni pamoja na Vital'O kutoka Burundi na APR ya Rwanda huku akisema zinatarajiwa kuwasili Zanzibar kesho.

Aliongeza kiingilio cha juu katika mechi zote zitakazochezwa kuanzia saa 10:15 jioni kitakuwa Sh. 5,000 na cha chini Sh. 3,000 na michezi ya jioni kiingilio cha juu kimepangwa kuwa ni Sh. 10,000 huku cha chini kikiwa ni Sh. 3,000.

Timu kutoka Tanzania Bara zitakazoshiriki michuano hiyo ni pamoja na Yanga, Simba, Azam FC zote za Dar es Salaam na Singida Fountain Gate kutoka mkoani Singida.

Singida Fountain Gate inatarajia kuondoka Dar es Salaam kesho wakati kikosi cha Yanga kinatarajia kutua visiwani humo Jumamosi tayari kujiandaa kuwania taji la michuano hiyo.

Wekundu wa Msimbazi, Simba wao wanatarajia kuondoka Dar es Salaam Jumapili wakati Kocha Abdulhak Benchikha, atakuwa akiongoza kwa mara ya kwanza kikosi chake katika michuano hiyo.

Hata hivyo, Simba na Yanga itawakosa wachezaji wake wa kikosi cha kwanza ambao wameitwa katika timu za taifa

INAENDELEA UK 23

# Simba SC, Yanga zaandaa 'suprise'

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha dogo la usajili likiwa limeshafunguliwa, Yanga imesema kama mambo yakienda vyema, itawatambulisha baadhi ya wachezaji wake wapya katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi, kauli hiyo pia ikitolewa na watani zao, Simba.

Yanga itaanza kampeni ya michuano hiyo Desemba 31, mwaka huu kwa kuwavaa Jamhuri wakati Januari Mosi, mwakani JKU itawakaribisha Simba na keshokutwa mechi za ufunguzi itakuwa ni kati ya Mlandege dhidi ya Azam FC na Vital'O itawaalika Chipukizi.

Meneja wa Yanga, Walter Harrison, alisema wanataka kufanya sapraizi kwa mashabiki wa soka Zanzibar kwa kuwatambulisha wachezaji wapya ambao wamesajiliwa katika kipindi cha dirisha dogo la usajili.

Alisema wanatarajia kuwatambulisha wachezaji ambao wamewasajili kuisaidia timu hiyo kufanya vizuri katika michuano mbalimbali ikiwamo Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Nawaambia wananchi wajiandae kwa sababu tunaenda Zanzibar kuhakikisha tunakuwa na ushiriki mzuri, tunachukua kombe, safari hii tunakuja tofauti kabisa tukiwa na malengo ya kuwapa burudani mashabiki wetu, tumedhamiria kutwaa ubingwa na wajue tu Zanzibar safari hii tunakuja na 'sapraizi' ya wachezaji wapya," alisema Harrison.

Tayari Yanga imeshatangaza kumsajili, Shekhan Hamisi Ibrahim, kutoka JKU ya Zanzibar.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema ni kweli anahitaji straika, lakini ni ngumu sana kwa kipindi hiki cha dirisha dogo kupata mshambuliaji mwenye ubora mkubwa.

"Sio sisi tu Yanga bali dunia nzima mahitaji wa mastraika asilia ni makubwa sana na hata Real Madrid wanahitaji pia. Ni kweli tunahitaji, lakini kwa kipindi hiki cha dirisha dogo ni ngumu sana, wachezaji wazuri wengi wako kwenye vikosi vinavyocheza

INAENDELEA UK 23



Kiungo wa Yanga, Maxi Nzengeli (kushoto), akijipanga kumtoka nyota wa Tabora United, Najim Mussa, katika mechi ya Ligi Kuu iliyochezwa Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >